Jumamosi Juni 15, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581708
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Waandishi** wafundwa miiko, maadili ya uchaguzi

UKURASA 2



**Wanahabari** wataka uwazi tuhuma kuhusu mmiliki wa blog

UKURASA 3



**TPA** sasa ruksa kukusanya tozo miundombinu ya bandarini

UKURASA 5



UK. 22

## UNITED KUWEKA KIKOMO MADARAKA YA TEN HAG



Dk. Deusdedit Ndilanha

Dk. Mwigulu Nchemba

MAONI BAJETI

# Madaktari wachekelea kikokotoo cha mafao

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA 8

**KONGAMANO LA UWEKEZAJI LAGOS KUONGEZA UWEKEZAJI**

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC), kimesema mabadiliko makubwa ya kisera na sheria yanayoendelea kufanywa na serikali ya awamu ya sita yamekuwa kivutio kikubwa kwa mitaji kutoka nje ya nchi...

RIPOTI MAALUM

## Tanzania ina walimu 68 tu somo la Uraia

• **Ni** wenye sifa za kufundisha hadi kidato cha nne ... *ukurasa 4*



Baadhi ya abiria wakishuka kwenye treni ya mwendokasi ya TRC, baada ya kuwasili katika stesheni ya mjini Morogoro wakitokea mkoani Dar es Salaam jana, ambapo safari ya treni hiyo ilitumia saa 1:45 tu. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

## Abiria wafurahia muda mfupi safari treni ya mwendokasi

UK. 3

**MICHEZO** **AZIZ KI, DIARRA KUIFILISI YANGA** UK.24

**MAONI,** UK.6



Wafanyabiashara wadogo wakiwa wamejenga vibanda vyao chini ya transfoma ya kupooza umeme mkubwa katika eneo la Kitunda Relini, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa maisha yao na wateja endapo itatokea hitilafu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madaktari kicheko kikokotoo mafao

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Madaktari Tanzania (MAT), kimetoa neno kuhusu kikokotoo cha wastaafu baada ya serikali kutangaza kuongeza mafao ya mkupuo kwa wastaafu na kueleza kuwa matamanio yao yalikuwa ni ongezeko kwa asilimia 50.

Juzi, serikali ilitangaza kwamba, watumishi ambao ni wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) sasa watapata mafao ya mkupuo kwa kikokotoo cha asilimia 40 badala ya asilimia 33 iliyoibua malalamiko.

Wenzao wa sekta binafsi walioko Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) nao wanatarajia kushuhudia ongezeko la mafao ya mkupuo, wakiwa na kikokotoo kipya cha asilimia 35 badala ya asilimia 33 iliyopo kisheria hivi sasa.

Katika maoni yao, siku moja baada ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kuwasilisha bungeni mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25, Rais wa MAT, Dk. Deus Ndilanha, alisema wanashukuru kufikia asilimia 40, ingawa walitamani kingefikia asilimia 50.

Dk. Ndilanha alisema wanatamani ingekuwa kwa asilimia 50 kwa kuwa umri wa madaktari bingwa kustaafu umeongezwa ikilinganishwa na watumishi wengine wa umma.

"Kwanza ifahamike kwamba madaktari ni sehemu ya watumishi wa umma na walioko sekta binafsi bahati mbaya na wao waliingia kwenye hiyo kadhia ya kushuka kwa kiwango cha mafao baada ya kustaafu.

"Kwa kweli walikuwa wanatamani sana kikokotoo kingebaki kama ilivyokuwa zamani asilimia 50 kwa fedha ya mkupuo, lakini kwa asilimia 40 tunashukuru, hoja yao kubwa ya madaktari umri wa kustaafu umeongezwa daktari bingwa umri wa kustaafu kwa lazima ni miaka 65 na kwa hiari ni 60.

"Tofauti na watumishi wengine wao kwa hiari ni miaka 55 kwa lazima ni umri wa miaka 60, utaona ni miaka mitano imeongezwa kwa madaktari, sasa alikuwa akistaafu kikokotoo chake ni asilimia 33 kilikuwa kinawaumiza zaidi kulinganisha na watumishi wengine," alisema.

Dk.Ndilanha alisema asilimia 40 si mbaya lakini matamanio ya madaktari ingekuwa ni asilimia 50 ingekuwa nzuri zaidi.

"Hata hii asilimia 40 tunashukuru kwani inahakikisha hawa watu wanapata chao baada ya kutumikia serikali na umma muda wote mpaka wanastaafu," alisema.

MAONI YA BAJETI

Kampuni ya kimataifa ya huduma za ukaguzi wa kitaalamu ya Ernst & Young (EY) imeonya kuhusu utegemezi wa fedha za wafadhili kutoka nje kuendesha miradi ya kimkakati ya maendeleo.

Meneja Mwandamizi wa Kodi kutoka EY, Fred Lugangira, alisema bajeti hiyo ni jumuishi kwa kuwa serikali imeweka malengo ya kimkakati na ubunifu ili kupanua wigo wa kodi na kuwezesha ulipaji wa kodi kwa hiari.

"Bajeti iliyowasilishwa inategemea mapato ya nje, ingawa suala hili haliepukiki, bado linahitaji kuchukuliwa kwa tahadhari kwa kubuni vyanzo vingi vya mapato kama ambavyo waziri amefanya. "Waziri tayari amependekeza kuwa mamlaka za serikali za mitaa kubuni vyanzo vingi vya mapato ili kupunguza utegemezi wa mapato kutoka nje, huu ni mpango mzuri tunaposonga mbele," alisema.

Aidha, alisema wameona namna kampuni za kimataifa zinavyosajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kulipa kodi, lakini pia mikakati iliyowekwa na serikali ya kupata mikopo yenye masharti nafuu ili kufadhili miradi ya maendeleo.

Pia alisema ajali za barabarani ni miongoni mwa maeneo ambayo serikali imekuwa ikipoteza nguvu kazi na kwamba, bajeti imependekeza ongezeko la faini za makosa ya barabarani hasa yanayohusu mauaji ili kuzipunguza, akisema hiyo ni hatua nzuri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya EY Tanzania, Joseph Sheffu, alisema bajeti hiyo ni shirikishi, lakini wasitegemee ilete mapinduzi kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi.

"Kasi ya kufufua uchumi ni mchakato, kwa hiyo tunatakiwa kuwa makini kwa kuufanya uchumi kuwa endelevu," alisema.

Alisema agenda ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu nishati safi ya kupikia imefanya bajeti hiyo kuwa kinara kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambayo ni tishio kwa ukuaji uchumi.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Innocent Donald, alisema bajeti hiyo inalenga kuhusisha sekta binafsi kwenye maendeleo ya nchi.

Naye Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Buberwa Kaiza, alisema bajeti ameisoma na kubaina matumizi ya watawala ni mengi kuliko ya watu wa kawaida katika mambo ya maendeleo.

"Shughuli za watawala, posho, mishahara, kusafiri, mafuta inaonekana karibu nusu ya bajeti nzima ila sio jambo jema halifurahishi kwa watu walio wengi tungependa bajeti iwe sehemu kubwa ya fedha za serikali iende kwenye maeneo ambayo yanayogusa watu wengi kama kilimo," alisema Kaiza.

Alisema sehemu ya fedha iende kwenye shughuli za nchi ambazo zinahusisha watu wengi kuna vijiji havina mawasiliano, hivyo vikiwezeshwa itasaidia mazao yanayozalishwa kujua soko lilipo.

Kaiza alisema inahitajika kutengwa kwa fedha za kuwawezesha wawekezaji katika kilimo kuongeza maghala ya kuhifadhi mazao na barabara za vijini kuwekwa lami ili kurahisha usafirashaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Maendeleo ya Jamii na Uchumi (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema bajeti hiyo imezingatia baadhi ya maoni, malalamiko na mahitaji ya wananchi.

"Katika maeneo hasa ya uzalishaji kwenye kilimo na kuangalia namna bora ya kuhamasisha, kupunguza uuzaji nje wa malighafi na kusisitza kuongeza thamani ndani ya nchi lakini pia kujaribu kupanua wigo wa ulipaji wa kodi yaani kuongeza walipa kodi wengi ili kupunguza mzigo kwa watu wanaolipa kodi," alisema

Aidha, alisema kuongezeka kwa kiwango cha kuwalipa wastaafu imeongezeka kidogo kwa kuwa kuna uwekezaji wa fedha hizo unapaswa kuongeza thamani ya michango ya wanachama ili waweze kupata kipato ambacho baada ya kustaafu wapate kiasi kikubwa cha fedha zao.

"Fedha hizo wamekuwa wakizichanga na kuziwekeza kwa muda mrefu zimeongezeka na kuzaa mfumo wa usimamizi wa hizo taasisi zinazosimamia mifuko ya hifadhi ya jamii inapaswa kubadilika," alisema.

**IMEANDALIWA na Beatrice Shayo na Romana Mallya**

# Waandishi wafundwa miiko, maadili ya uchaguzi

**Na Restuta James**

SERIKALI imewasisitiza waandishi wa habari kuzingatia miiko na maadili ya uandishi wa habari wakati wa mchakato wa uchaguzi na baada ya kumalizika kwa mchakato huo ili kuhakikisha nchi inabaki kwenye amani na utulivu.

Akizungumza kwenye mafunzo ya waandishi wa habari yaliyoandaliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Msaidizi katika Idara ya Habari Maelezo, Patrick Kipangula, alisema waandishi na vyombo vya habari vina jukumu la pekee kuhakikisha nchi inabaki na amani, utulivu na mshikamano kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Alisema hilo litawezekana kama wagombea na vyama vya siasa vitapewa nafasi sawa ya kutangaziwa habari zake bila upendeleo.

Kipangula aliwataka waandishi kuzingatia ukweli, uadilifu, uaminifu, weledi na usahihi wa taarifa na kuepuka rushwa pamoja na kuheshimu faragha za watu.

"Tuepuke taarifa ambazo zinaweza kuvunja amani na usalama wa nchi. Tunatakiwa kuhakikisha Taifa letu linabakia tulivu na salama wakati wote wa mchakato na baada ya uchaguzi," alisema.

Kadhalika, amewataka kuchukua tahadhari na kuthibitisha taarifa kabla ya kuitangaza au kuichapisha, kwa kuwa baadhi ya watu wanaweza kutumia akili mnemba kutengeneza picha zenye nia ovu dhidi ya vyama au baadhi ya wagombea.

Awali, Meneja wa Huduma za Utangazaji kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Andrew Kisaka, alisema vyombo vya habari vinaaminika na jamii na hivyo vina nafasi ya kuunganisha nchi kwenye masuala yote ya kitaifa na maendeleo.

Alisema wakati huu wa zoezi la kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura, waandishi na vyombo vya habari wanao uwezo wa kuwapa wananchi taarifa za faida za kujiandikisha na kupiga kura.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, Mtibora Selemani, alisema INEC itatoa ushirikiano kwa vyombo vya habari na wadau wote wa tume wakati wa uboreshaji wa daftari na kwenye mchakato wa uchaguzi.

Kwa mujibu wa INEC, maboresho ya daftari la kudumu la wapiga kura yanatarajiwa kuzinduliwa Julai Mosi, mwaka huu mkoani Kigoma.

Juzi, Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele, aliwataka wanahabari kutumia fani yao kuwahamasisha wananchi kujiandikisha kwenye daftari la wapigakura.

"Tume inataajia ushirikiano mkubwa kutoka kwenu kwa kuwafikishia wananchi taarifa sahihi na kwa wakati zinazohusu zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura," alisema.

## HABARI KITAIFA



Meneja wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Mikocheni, Dk. Fred Tairo akionyesha kwa Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ally (kushoto), baadhi ya magonjwa yanayosumbua zao la nazi, wakati wa hafla maalumu iliyoandaliwa na TARI kwa lengo la kuwaongezea uelewa wakulima wa zao hilo kuhusu namna ya kulima kisasa na kuongeza tija katika uzalishaji wa wilayani humo mkoani Pwani mapema wiki hii. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Abiria 1,400 wasafiri bure treni ya SGR, wafurahia kutumia muda mfupi

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

ZAIDI ya abiria 1,400 wamesafirishwa bila malipo kwa treni ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro na kisha kurejea huku wakifurahia kutumia muda mfupi.

Ujenzi wa reli hiyo inayoaminika ni ndefu kwa Afrika yenye kilometa 300 ya kisasa itawezesha abiria kusafiri kwa gharama nafuu.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, ambaye alikuwa miongoni mwa wasafiri wa treni jana, alisema baada ya kuwasili kwenye kituo cha Morogoro kuwa treni hiyo imetumia saa 1:45 baada ya kutoka Dar es Salaam saa 12:10 na kufika Morogoro saa 1:55 asubuhi.

"Hili ni jambo la kihistoria na kutokana na furaha hii, wakati tunatoka Dar es Salaam Rais Samia Suluhu Hassan, ametuelekeza na Mkurugenzi ameanza kulitekeleza.

"Wale watakaosafiri leo (jana) kama ishara ya kusherekea ameelekeza watapanda bure kwa hiyo waliopanda kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro na kurudi Dar es Salaaam amelipia yeye nauli kama shukrani," alisema.

Kihenzile alisema kwa mara ya kwanza Tanzania imeanza safari za treni hiyo ya kisasa ambapo awali watanzania walitegemea treni za TAZARA pekee ambayo ina kilometa 1400 kutoka Dar es Salaam hadi Kapilimposh.

Alisema kwa Afrika, Tanzania ndio nchi pekee ambayo inajenga reli ndefu zaidi ya kisasa ambapo kwa kimataifa nchi kama China wana takribani kama kilometa 40,000, Hispania kilometa 3900, Japani kilometa 3700 na Ufaransa kilometa 2700 ambapo inayofuatia Tanzania ikishika nafasi ya tano," alisema.

Aidha, alisema Tanzania ndiyo nchi pekee kwa Afrika iliyojenga reli ndefu ya kisasa na ya gharama nafuu ambayo inafungua uchumi kati ya nchi na nchi inazopakana nazo.

"Reli hii ni faida kwa wananchi wetu kutoka Dar es Salaam treni hii waliyokuja nayo ni Sh. 13,000 ambayo mwananchi wa kawaida anaiweza na kwenda mpaka Dodoma ni Sh. 30,000 na mwananchi anaweza kuwahi na akaenda kufanya shughuli zake na kurudi alipotoka," alisema Kihenzile.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema Watanzania wengi walilisubiri jambo hilo kwa hamu.

Kadogosa alisema watanzania wana haki ya kujivunia kwa kuwa inawezekana wakayaona ya kawaida, lakini si mambo ambayo yanatokea katika nchi zingine.

Alisema wananchi wananafasi kubwa ya kutumia reli hiyo katika shughuli za maendeleo ili kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Kadogosa alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza ahadi yake aliyoitoa bungeni ya kumalizia mradi wa ujenzi wa reli hiyo ikiwa ni sehemu ya miradi aliyoikuta wakati akiingia madarakani ikiwa chini ya asilimia 50.

"Alichokifanya Rais Samia ni kukamilisha ahadi za utekelezaji wa miradi na kitendo hicho ni kumuenzi mtangulizi wake, Hayati Dk. John Pombe Magufuli, kama kazi aliyoanzisha ameikamilisha kama alivyowaahidi Watanzania," alisema.

Kadogosa alisema treni hiyo yenye mabehewa ya kawaida na kibiashara ina mabehewa 14.

Mwenyekiti wa Bodi ya TRC, Ally Karavina, aliwaomba watanzania kuzingatia muda wakati wa kupata huduma hiyo kwa kuwa inakwenda na muda uliopangwa tofauti na usafiri mwingine ikiwamo treni iliyozoeleka ya reli ya kati.

Alisema shirika linaweza kuongeza treni nyingine kulingana na mahitaji ya soko kwa kuwa na treni zinazokwenda Dar es Salaam na nyingine zinarudi Morogoro zikipishana ambapo abiria watapata huduma za kisasa.

Inda Mhando, ambaye alikuwa mmoja wa abiria katika treni hiyo, alisema usafiri huo umemwamasisha kusafiri zaidi kwa kuwa ni moja pia ya utalii wa ndani.

Naye Mohamed Khasim, alisema usafiri huo akilinganisha na mabasi, unaokoa muda wa msafiri kwa kufika haraka.

Ujenzi wa reli hiyo ya kisasa ulianza rasmi Aprili, 2017 na katika awamu ya kwanza, umekamilika kipande cha Dar es Salaam - Morogoro na awamu ya pili, Morogoro hadi Dodoma na awamu zingine ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwamo Dodoma (Makutopora) - Tabora, Tabora- Isaka na Isaka-Mwanza.

# Wanahabari wataka uwazi wa tuhuma zinazomkabili mwenzao

**Na Timothy Itembe,**
MUSOMA

UONGOZI wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mara (MRPC) umeliomba Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kuweka wazi tuhuma zinazomkabili mwandishi wa habari wa Blog ya Dima Online, Dinna Maningo.

Katika taarifa yake jana kwa vyombo vya Habari, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Mugini Jacob, alisema wana imani na Jeshi la Polisi mkoani humo litatoa taarifa kuhusu tuhuma zinazomkabili mwandishi huyo bila kuchelewa.

Jacob alisema Dinna alikamatwa juzi saa 2:00 usiku akiwa nyumbani kwake, Mtaa wa Kokegohoma, Halmashauri ya Mji wa Tarime, wakati akijiandaa kulala na familia yake. Askari kutoka Mwanza wakishirikiana na polisi wa Kituo cha Tarime walidaiwa kufika na kumkamata.

"Mara tu baada ya kukamatwa kwa Dinna, nilipata taarifa na nilifika Kituo cha Polisi Tarime tukiwa na waandishi wenzangu wawili, Godfrey Marwa na Timothy Itembe. Tulifika na kumwona hali yake ya kiafya ilikuwa nzuri na hakutaja sababu inayofanya kushikiliwa na polisi," alisema.

Punde baada ya kumsalimia, alichukuliwa kituoni hapo na askari na kupelekwa Nyamongo na kufanya upekuzi kwa masuala yao wanayoyataka katika ofisi yake na kumpeleka usiku Kituo cha Polisi cha Bomani, Tarime na jana kusafirishwa mkoani Mwanza.

Mwenyekiti huyo alisema wanaendelea na mawasiliano na uongozi wa Mwanza Press Club ili kusaidia kufuatilia tukio hilo pindi atakapofikishwa jijini humo.

"Tuna imani Jeshi la Polisi litafanya kazi yake kwa weledi ili haki iweze kutendeka kwa wakati," alisema Jacob.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Kamishna msaidizi mwandamizi (SACP) Wilbrod Mutafungwa, alipotafutwa na Nipashe ili kuzungumzia kuhusu kukamatwa kwa mwandishi huyo, aliomba atumiwe ujumbe mfupi ambao hata alipotumiwa, hakujibu.

RIPOTI MAALUM

# Nchi ina walimu 68 tu wa somo la Uraia

## -Ni wenye sifa za kufundisha hadi kidato cha nne Tanzania Bara...

**Na Francis Kajubi**

KATIKA shule za sekondari za serikali Tanzania Bara kuna walimu 68 pekee wenye sifa za kufundisha somo la Uraia, mwandishi wa habari hii amebaini.

Hao ndiyo wanaostahili kuwafundisha somo hilo wanafunzi wote wa kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule za umma za sekondari nchini.

Hata hivyo, kutokana na uhaba uliopo, walimu wasio na sifa za kufundisha Uraia, ndiyo wanabeba jukumu kufundisha somo hilo katika shule hizo za umma.

Athari za uhaba huo ni kushuka ufaulu wa somo hilo kwa kasi unaoonekana kwenye matokeo ya upimaji kidato cha pili na Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne.

Uchunguzi wa kitakwimu umebaini kuwapo wanafunzi wanaopata daraja "A", "B+" au "B" katika masomo ya Hisabati, Fizikia na Kemia lakini wanaangukia daraja "C", "D" au "F" katika somo la Uraia.

Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, walimu wa somo la Uraia katika shule za sekondari ni wale ambao wamehitimu shahada au stashahada ya ualimu kwa kulisoma somo la Sayansi ya Siasa vyuoni kama somo mahususi watakalofundisha shuleni.

Ripoti ya Upimaji wa Wanafunzi wa Kidato cha Pili 2022 (FTNA 2022) ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo mwandishi ameiona, inabainisha kuwa hadi Aprili 2022, Tanzania ilikuwa na walimu 66 pekee waliosoma Sayansi ya Siasa kama somo mahususi la kufundisha katika shule za sekondari.

Walimu hao ndiyo wenye sifa ya kufundisha somo la Uraia waliokuwa katika shule za sekondari za serikali hadi wakati huo (Aprili 2022).

Hata hivyo, mwandishi anafahamu kwamba idadi yao iliongezeka hadi kufikia walimu 68 kufikia mwezi Februari mwaka huu.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mahitaji ya walimu waliosomea kufundisha somo la Uraia katika shule za sekondari mwaka 2022 yalikuwa walimu 15,816. Hata hivyo, mahitaji yaliongezeka kufikia walimu 16,695 Februari 2023, kwa mujibu wa FTNA 2023.

Ripoti (FTNA 2022) inaonesha wanafunzi 635,130 walisajiliwa kufanya mtihani wa upimaji wa kidato cha pili mwaka 2022, ingawa ni wanafunzi 633,095 waliofanya mtihani wa somo hilo. Kati yao, 436,094 (asilimia 68.88) walipata daraja "F" katika somo hilo.

Kwa mujibu wa Baraza la Mitihani (NECTA), wanafunzi 125,788 (asilimia 19.87) walipata daraja "D", 59,995 (asilimia 9.48) walipata daraja "C", 8,058 (asilimia 1.27) walipata daraja "B" na 3,160 (asilimia 0.5) walipata daraja "A".

Katika Shule ya Sekondari Goba Mpakani, mkoani Dar es Salaam, wanafunzi 304 walifanya mtihani huo. Kati yao, mmoja alifaulu kwa daraja "C", 41 walipata daraja "D" na wanafunzi 262 walifeli, kwa maana walipata daraja "F".

Hata hivyo, matokeo ya mtihani huo wa upimaji wa kitaifa kidato cha pili, yanaonesha asilimia 57 ya wanafuzi



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda. **PICHA: MTANDAO**

waliopata daraja "F" katika somo la Uraia katika shule hiyo walipata daraja "B+", "B" na "C"katika masomo ya Hisabati, Fizikia na Kemia.

Joseph Kiriri, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Goba Mpakani, anasema shule inao walimu wanne wanaofundisha somo la Uraia; mmoja ndiye amesomea kufundisha somo hilo.

"Mmoja amesomea kufundisha somo la Fasihi ya Kiingereza, mwingine somo la Kiswahili na mwingine somo la Historia, ila wote wanafundisha Uraia. Hii ndiyo sababu kuu wanafunzi kufeli somo hili," anasema Mwalimu Kiriri na kueleza kuwa shule inavyo vitabu vingi vya somo la Uraia katika maktaba yake kulinganisha na masomo mengine.

Anasema upungufu wa walimu wa Uraia unachangiwa na kutokupandishwa vyeo walimu wa somo hilo kwa muda mrefu hata kama sifa wanazo, jambo linalofanya wengi wao kuacha kufundisha na kuingia katika siasa.

Mwalimu Joyce Mbise wa Shule ya Sekondari Goba Mpakani, anasema amesomea kufundisha Historia, lakini anafundisha Uraia shuleni huko kutokana na uhaba wa walimu uliopo.

Anasema alianza kufundisha shuleni huko mwaka 2013 baada ya kuhitimu Stashahada ya Ualimu katika Chuo cha Ualimu Songea.

"Ilinichukua mwaka mzima kujifunza na kuzoea kufundisha Uraia. Ninafundisha mikondo mitano, kila mmoja ukiwa na wanafunzi kati ya 55 hadi 65," alisema Mwalimu Joyce.

Hata hivyo, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 iliyofanyiwa mapitio mwaka jana, inaelekeza shuleni kuwe na uwiano wa 1:45 (yaani mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45). Hivyo, Mwalimu Joyce amebeba mzigo wa ziada.

Grace Mwaisabila ni mwalimu pekee aliyesomea kufundisha somo la Uraia shuleni Goba Mpakani. Alihitimu Shahada ya Elimu mwaka 2009 katika Chuo cha Ualimu Mkwawa.

Anasema kuwa baada ya kuhitimu alipangwa kufundisha somo la Uraia kidato cha I-IV katika Shule ya Sekondari Kilakala, mkoani Morogoro.

"Pale shuleni nilikuwa mwalimu pekee aliyesomea kufundisha Uraia. Walimu wenzangu wawili; mmoja alikuwa amesomea kufundisha Historia na mwingine Jiografia, lakini wote tulikuwa tunafundisha somo hilo (Uraia)," anasema.

Mwalimu Grace anasema alihitimu chuoni Mkwawa pamoja na wenzake takribani 300 waliosomea Sayansi ya Siasa. Baadhi walichagua kuendelea na elimu ya juu zaidi huku wengine wakitafuta kazi ya kufundisha katika shule za sekondari zinazomilikiwa na watu na taasisi binafsi.

Kwa mujibu wa ripoti ya Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022 ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tanzania Bara ina jumla ya shule za sekondari 5,592. Hata hivyo, ripoti hiyo haibainishi ni shule ngapi zinamilikiwa na serikali.Uraia si somo pekee lenye uhaba wa walimu katika shule za sekondari za umma Tanzania Bara. Ripoti ya FTNA 2022 inaonesha kuwapo uhaba wa walimu wa Kiingereza 11,337 (asilimia 47).

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mahitaji yalikuwa walimu 21,435 hadi kufikia Desemba 2022, lakini walimu wa Kiingereza waliokuwapo ni 11,337.

Ni upungufu unaotajwa kuchangia asilimia 40 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani wa upimaji wa kidato cha pili mwaka 2022 kupata daraja "F" katika somo hilo.

**JEDWALI LA UHABA WA WALIMU**

| Somo | Mahitaji | Waliopo | Upungufu % |
|---|---|---|---|
| Historia | 17,318 | 15,960 | 1,358 8 |
| Jiografia | 18,181 | 13,755 | 4,426 24 |
| Kiswahili | 16,792 | 15,828 | 964 6 |
| Fasili (Eng) | 2,964 | 30 | 2,934 99 |
| Kiingereza | 21,435 | 11,337 | 10,098 47 |
| Baiolojia | 17,813 | 5,795 | 12,018 67 |
| Kemia | 16,664 | 6,074 | 10,590 64 |
| Fizikia | 16,334 | 3,758 | 12,576 77 |
| Hisabati | 19,216 | 5,537 | 13,679 71 |
| Uraia | 15,816 66 | 15,750 | 99.6 |

**Hali ya upungufu wa walimu katika shule za sekondari za umma kidato cha I-IV. CHANZO: FTNA 2022.**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, anathibitisha kuwapo changamoto ya upungufu wa walimu nchini, akieleza kuwa wizara imeandaa mwongozo wa walimu kujitolea ili kuziba upungufu huo.

"Tumekwishaanza kuchukua hatua kukabili changamoto ya upungufu wa walimu si tu katika shule za sekondari, bali pia katika ngazi zote za elimu. Mojawapo ya hatua hizo ni kuandaa mwongozo wa walimu wa kujitolea," anasema Prof. Mkenda.

Mwandishi wa habari hii ameona nakala ya mwongozo huo uliopewa jina la "Mwongozo wa Walimu wa Kujitolea katika Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Tanzania Bara wa Juni 2023".

Utangulizi wa mwongozo huo unabainisha kuwa hadi mwezi Machi 2022 kulikuwa na jumla ya wanafunzi 14,853,242 katika ngazi zote za elimu Tanzania Bara. Kati yao, 1,433,779 ni elimu ya awali, 10,873,782 wa shule za msingi, 2,530,651 wa sekondari na 15,030 wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mwongozo huo unabainisha kuwa katika ngazi zote tajwa kulikuwa na walimu 270,614. Kati yao, 10,134 ni wa elimu ya awali, 170,730 wa shule za msingi, 89,500 wa sekondari na 250 wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

"Hata hivyo, mahitaji ya walimu katika ngazi zote tajwa za elimu ni 538,060. Hii inaashiria kuwapo upungufu wa walimu 267,446," unabainisha mwongozo huo.

Mwongozo huo unabainisha taratibu ambazo waombaji watazipitia ili kupata nafasi za kufundisha kwa kujitolea huku ukisema kuwa maslahi yao yataamuliwa na halmashauri husika.

Kwa mujibu wa mwongozo huo hadi mwezi Julai 2022, kulikuwa na walimu wa kujitolea 17,237 nchi nzima. Kati yao, walimu 10,373 walikuwa katika shule za msingi, 6,542 walikuwa katika shule za sekondari na 322 walikuwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Kimsingi, uhaba wa walimu shuleni unakwaza utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26).

Mpango huo pamoja na mambo mengine umebainisha malengo muhimu katika sekta ya elimu yanayotakiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2026, ambayo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari na kuboresha uwiano wa walimu na wanafunzi katika ngazi zote.

Hali hiyo pia inakinzana na Katiba ya nchi, Ibara ya 11(2) inayoelekeza utoaji haki ya kujielimisha katika fani ambayo kila raia anao uhuru kufikia upeo anaotaka kulingana na stahiki na uwezo wake.

***ITAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA



Wafanyabiashara katika Soko la Ilala Karume jijini Dar es Salaam, wakiwa wamepanga bidhaa zao katika eneo la waenda kwa miguu na kuwalazimu wapita njia kutumia barabara yenye magari mapema wiki hii, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TPA ruksa kukusanya tozo miundombinu bandari

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeamua kuirejeshea Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), jukumu la kukusanya tozo inayotokana na matumizi ya miundombinu ya bandari (wharfage) ili kuiwezesha kuboresha shughuli zake.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo juzi wakati akiwasilisha mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya serikali jijini Dodoma. Awali, fedha hizo zilikuwa zinakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema fedha ambazo TPA itakusanya zitawekwa kwenye mfuko maalum wa TPA ulioko Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na matumizi yake yatafanyika baada ya kuomba na kupata idhini ya mlipaji mkuu wa serikali.

Dk. Nchemba alisema lengo la uamuzi huo ni kuiwezesha mamlaka hiyo kupata fedha kwa wakati kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bandari na kuongeza ufanisi wake.

"Mheshimiwa Spika, napendekeza marekebisho ya Sheria ya Bandari ya mwaka 2004 ili kurejesha jukumu la kukusanya tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari," alisema.

Mmoja wa wadau wa bandari, Maulid Ismail, alipendekeza kuwa wakati wa kuandaa malipo hayo ya tozo ya bandari (wharfage), serikali ihakikishe mifumo ya TPA na TRA inasomana ili kuhakikisha wateja wanalipa malipo halali na sahihi. "Tuhakikishe mifumo ya mamlaka hizi mbili, yaani TRA na TPA, inasomana ili kuhakikisha wateja wanalipa malipo sahihi na halali bila kuonea mtu au kupoteza mapato na hili likifanyika litasaidia sana udhibiti wa ukwepaji wa kodi na tozo," alisema Ismail.

Akizungumza wakati wa kupokea gawio kwa mashirika ya umma hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, alielezea kuridhishwa na mafanikio ambayo TPA imeyapata hadi kuongoza katika taasisi zilizotoa gawio serikalini kwa kutoa Sh. bilioni 153.

Rais Samia alisema uwekezaji ambao umefanywa na serikali kwenye mamlaka ya bandari umeanza kulipa licha ya kelele za baadhi ya waliokuwa wakipinga uwekezaji huo.

Mtaalamu wa masuala ya bandari nchini, Emmanuel Mallya, hivi karibuni alisema kwa serikali kutoruhusu TPA kukusanya wharfage ni sawa na kuizuia kukua na kukwamisha ongezeko la ufanisi unaoletwa na uwekezaji toka sekta binafsi.

Mallya ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Chama cha Mawakala wa Meli Tanzania (TASAA), anasema ni vyema TRA ikaendelea na majukumu yake ya kukusanya kodi ambayo sehemu kubwa inatokana na ufanisi wa huduma za bandari.

"Sasa kama unataka ukusanye kodi zaidi, lazima uiache bandari iwe na uwezo wa kujiendesha na kuboresha miundombinu na huduma nyingine nyeti zilizo ndani ya mamlaka," alisema.

Wakichangia bajeti ya Wizara ya Uchukuzi hivi karibuni, baadhi ya wabunge walisema ili TRA iweze kukusanya kodi zaidi, inabidi TPA iachwe ikusanye wharfage kwa ajili ya kuboresha miundombinu yake, huduma na usalama bandarini.

Kwenye mjadala huo, Mbunge wa Viti Maalumu, Esther Maleko, alisema pamoja na kazi nzuri inayonywa na TPA chini ya Mkurugenzi wake Mkuu, Placidius Mbossa, serikali iiruhudu mamlaka hiyo kukusanya tozo ya matumizi ya miundombinu (wharfage).

# TLS yawafunda wenye ulemavu, wanavyuo umuhimu katiba mpya

**Na Grace Mwakalinga**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimeanza kuwajengea uwezo makundi mbalimbali katika jamii wakiwamo wenye ulemavu, wanavyuo na wanawake juu ya umuhimu wa kupata katiba mpya.

Katika kufanikisha azma ya kuwajengea uwezo makundi hayo, TLS inaendesha mijadala ya wazi kwa kutoa nafasi kujadili mapungufu na mahitaji yao ili yaingizwe kwenye katiba mpya ambayo imetajwa kukidhi mahitaji kwa wananchi. Akizungumza jana katika mafunzo hayo ya siku mbili yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TLS, Mariam Othman, alisema wapo tayari kukusanya maoni na kuheshimu mawazo bila kujali itikadi za kisiasa, kidini, kijamii kwa kuwa kila mmoja ana mchango kwenye upatikanaji wa katiba mpya.

Mariam alisema miongoni mwa lengo ya kuanzisha mjadala huo ni kuongeza ushirikishwaji wa wananchi kueleza masuala wanayoyahitaji ili yaingizwe kwenye Katiba mpya. "Tumeanza kuendesha mijadala hii ya katiba mpya mwanzoni wa mwezi huu. Tayari tumetoa mafunzo kwa mikoa ya Mbeya, Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na Dodoma kwa kuyafikia makundi maalum, wanawake, viongozi na wanavyuo ili kutoa maoni yao kuhusu mabadiliko ya katiba mpya," alisema Mariam.

Mchambuzi wa Masuala ya Katiba, Deus Kibamba, alisema watu wenye ulemavu wanayo nafasi ya kuainisha masuala mbalimbali wanayoyahitaji ili yaingizwe kwenye katiba mpya.

Kibamba alisema miongoni ni uboreshwaji wa miundombinu kwenye taasisi za umma na marekebisho ya sheria katika katiba ya sasa kuhusu kundi hilo.

Alisema TLS ni chombo muhimu ambacho kitaisaidia serikali kukusanya maoni mbalimbali ya wananchi kuhusu masuala ya kisheria na mambo ya kuingizwa kwenye mchakato wa katiba mpya.

"Yamefanyika marekebisho ya mara kadhaa ya katiba yetu tangu kuandikwa mwaka 1977, 1984 na 2005 sasa imekuwa na viraka maisha yanabalika kuna mambo ambayo yamepitwa na wakati, yanahitajika mengine kuingizwa kulingana na utu, haki na mazingira ya wananchi," alisema Kibamba.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Walioumia Uti wa Mgongo, Abdulaziz Shambe, alisema baadhi ya huduma na mahitaji hawayapati kwenye maeneo ya kutolea huduma, hivyo anaamini kupitia maoni aliyoyatoa yataingizwa kwenye katiba mpya.

Miongoni mwa wanafunzi walioshiriki mafunzo hayo akiwamo Diana Pallangyo, kutoka Chuo cha Usimamizi wa Biashara nchini CBE, alisema miongoni mwa mambo yanayopaswa kushughulikiwa ni suala la wananchi wa Tanzania Bara kupata uhalali wa kumiliki ardhi Tanzania visiwani Zanzibar.

# Temeke yaanza usafishaji wa damu

**Na Mwandishi Wetu**

Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke (TRRH) imeanza rasmi kutoa huduma za usafishaji damu (dialysis) ikiwa ni mara ya kwanza katika kuwahudumia wagonjwa wenye changamoto hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali, Dk. Joseph Kimaro, alithibitisha kuwa huduma hiyo ilianza jana huku akisema hiyo ilikuwa siku muhimu kwa hospitali kwa kuwa huduma hiyo imekuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu.

Alisema hospitali imepata mashine 10 za usafishaji damu zilizonunuliwa kwa kutumia mapato ya ndani.

Dk. Kimaro alisema huduma hiyo itasaidia wagonjwa wenye matatizo ya figo wanaoishi Temeke na maeneo jirani kama vile Kigamboni, Mkuranga na Pwani ambako hakuna hospitali inayotoa huduma kama hiyo.

Kwa mujibu wa Dk. Kimaro, utekelezaji wa huduma hii si tu hitaji la hospitali hiyo bali ni mpango wa serikali unaolenga kufikisha huduma za kibingwa na bingwa bobezi kwa wananchi. Huduma hiyo mpya, alisema itapunguza foleni na changamoto za umbali katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Dk. Kimaro aliishukuru Mamlaka ya Usimamizi wa bandari Tanzania (TPA) kwa kuwezesha ukarabati wa jengo la kutolea huduma hiyo na kununua televisheni zitakazosaidia wakati wa kutoa huduma.

Pia aliwataka wananchi kuendelea kufanya mazoezi na kufuata ushauri wa madaktari ili kupunguza magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa kuwa dawa zisipotumika kwa usahihi zinaweza kusababisha magonjwa kama ya figo.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Dk. Farida Ntonga, alishukuru uwapo wa mashine hizo na kusema timu ya madaktari na wauguzi wamepokea mafunzo ya kutosha, hivyo wananchi wawe na imani na wataalamu hao.

Alisema mwaka jana hospitali ilipokea wagonjwa takribani 200 ambao walihitaji rufani kwenda Muhimbili lakini sasa kutokana na huduma hiyo mpya, rufani hizo zitapungua na wagonjwa watapata huduma katika hospitali hiyo ya mkoa.

Humphrey Tarimo, baba mkubwa wa mgonjwa wa kwanza kuhudumiwa na mashine hiyo, alielezea furaha yake kwa huduma hiyo kusogezwa karibu na makazi yao.

Alisema walikuwa wakipata changamoto za usafiri kutokana na umbali wa hospitali, hivyo anaupongeza uongozi wa hospitali kwa ukarimu na utashi wao wa kujali wagonjwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi kuelekea msimu mpya yazingatie uhalisia

**WAKATI** mashindano ya Euro 2024 yakitarajiwa kufanyika kuanzia kesho, hapa nchini wachezaji wetu wanaoshiriki Ligi Kuu Bara, Ligi ya Championship, First League (zamani Ligi Daraja la Pili), na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyomalizika jana wako katika mapumziko.

Kalenda hii ya mapumziko kwa wachezaji haijawekwa ili kujifurahisha, imeandaliwa maalumu kuipa nafasi miili na akili za wachezaji muda wa kujitengeneza upya na kujiandaa tayari na msimu mpya wa mashindano.

Wachezaji wanatakiwa kuheshimu muda wa mapumziko kwa sababu ambaye hatapumzika, atakuwa katika changamoto mbalimbali pale watakaporejea katika maandalizi ya msimu mpya wa mashindano wa 2024/2025 ambao utafanyika kuanzia mapema Agosti, mwaka huu.

Kutumia mapumziko haya vibaya, si tu kutakutesa mchezaji husika wakati wa kuanza mazoezi ya msimu mpya, lakini nyota huyo anaweza kupoteza namba katika kikosi anachocheza kutokana na kuchelewa kuingia katika mfumo kwenye mechi za awali.

Kufanya starehe zaidi na mambo mengine yanayokatazwa kwa wachezaji, hili ni jambo ambalo linakumbushwa kwa kila mmoja kujichunga kwa sababu utimamu mzuri wa mwili ndio hupelekea kupata namba na kuisaidia timu yako kuanza vyema msimu husika.

Kuna baadhi ya wachezaji huachwa, hupoteza namba na wengine hulazimika kutolewa kwa mkopo katika timu nyingine na nafasi zao kuletwa wachezaji wapya kwa sababu tu hakuisaidia klabu yake kupata matokeo chanya wakati msimu mpya unaanza.

Inafahamika kuwa 'biashara asubuhi', kila timu huitaji kuvuna pointi tatu muhimu kuanzia mechi ya kwanza ili kujiweka mahali salama na kuelekea kutimiza malengo yake, na hili litatimia endapo wachezaji watajituza wakati wa mapumziko na kufanya maandalizi sahihi.

Haitakuwa vyema timu ikafanya maandalizi kwa 'kukurupuka' au kwa kufuata mkumbo kwa sababu wameona wapinzani wao wameamua kuweka kambi mahali fulani.

Umefika wakati wa kuzipa nafasi Idara za Ufundi kuamua aina ya mazoezi, mahali na michezo ya kirafiki ambayo itasaidia katika kukijenga na kukiimarisha kikosi husika na si kufanya kwa ajili ya kujionyesha.

Pia kumekuwa na utaratibu wa timu kuandaa mechi za kirafiki dhidi ya timu za ndani na nyingine kutoka nje ya Tanzania, lakini viongozi wamekuwa wakifanya uteuzi wa kualika klabu ambazo kiuhalisia haziwapi kipimo halisi kuelekea msimu mpya.

Tunazikumbusha timu ambazo zitaiwakilisha Tanzania Bara na Zanzibar katika mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, kucheza mechi za kirafiki zenye hadhi na timu watakazokutana nazo katika mashindano hayo ya kimataifa.

Kucheza mechi za kirafiki na timu ndogo, kiufundi unairudisha au unaichelewesha timu yako kuelekea katika mafanikio kwa sababu benchi la ufundi halitaona mapungufu yake sawa na badala yake watafurahia idadi kubwa ya mabao ambayo yatafungwa kwenye michezo hiyo.

Hongera sana Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kubadilisha mfumo wa kupata mshindi wa mashindano ya Ngao ya Jamii, ambapo msimu mpya tutashuhudia timu nne zilizofuzu michuano ya kimataifa kuanza kuonyesha makali yake katika mashindano hayo.

Baada ya kumaliza maandalizi ya msimu mpya, tunaamini makocha watakaokuwa na dhamana ya kuziongoza timu hiyo watatumia michuano hiyo kurekebisha makosa kabla ya kuanza kushiriki mashindano ya CAF ambayo mechi zake za awali zitafanyika kati ya Agosti 13 na 15, mwaka huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# VAR ije kusaidia waamuzi, na kamwe isiongeze utata

**SASA** ni rasmi Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza tangu historia yake, itakwenda kutumia mashine za mfumo wa video kusaidia marefa kufanya uamuzi sahihi uwanjani.

Hiyo ni baada ya serikali kupendekeza kutoa msamaha wa kodi katika uingizaji wa vifaa hivyo hapa nchini.

Katika Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25, aliyoisoma juzi Bungeni, Dodoma, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akipendekeza hayo alisema, uwepo wa VAR utaondoa malalamiko ya maamuzi yasiyo sahihi, kwa waamuzi kutoona vyema kutokana na kasi ya mchezo au upendeleo.

"Msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara tutaanza kutumia VAR ili kuhakikisha matokeo yanayopatikana uwanjani yanakuwa ya haki, ili tuwe nazo za kutosha katika viwanja vyote, ninaleta pendekezo la kutoa msamaha katika uingizaji mashine hizo na vifaa vyake kwa ufafanuzi utakaotolewa hapo baadaye, " alisema wakati akiwasilisha mapendekezo ya bajeti ya mwaka.

Tunaipongeza Serikali kwa kuwa sikivu, ambapo wamekuwa wakiyafanyia kazi haraka mambo mbalimbali ya kimichezo, na hata malalamiko ya mashabiki wa michezo nchini, hususan soka.

Kuwepo kwa VAR katika ligi yetu imekuwa ni kilio cha muda mrefu ili kupunguza malalamiko ya baadhi ya waamuzi, hasa ikihusu zinazoitwa 'timu kubwa' au 'timu pendwa'.

Tanzania itakuwa ni moja kati ya nchi chache sana Afrika kuwa na ligi ambayo itakuwa na usaidizi ya maamuzi ya kiteknolojia.

Hii inaonyesha vile vifaa vya VAR ambayo vinaletwa kwa msaada wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), itakayofungwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam haitatozwa kodi.

Miezi michache nyuma, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Wallace Karia, alibainisha moja wa wadhamini wa Ligi Kuu Tanzania wataleta VAR inayotembea, ambayo kitaalamu inaitwa 'mobile VAR.'

Akasema hii itakuwa inasafiri mikoani kwa ajili ya kufanya kazi katika viwanja mbalimbali kama itakavyoelekezwa na Bodi ya Ligi.

Karia amependekeza iwe inakwenda katika michezo yenye mvuto, inatazamwa na watu wengi, na mashabiki wengi pia.

Kwa hili lililofanywa na serikali, mashine hiyo nayo itaingizwa ikiwa ndani ya msamaha.

Nashauri pia taasisi zingine, wadau na wafanyabiashara, kuchangamkia fursa kwani wanaweza kununua na kuleta mashine hizo nchini, wakafanya biashara ya kuzikodisha ili zikafungwe katika viwanja mbalimbali.

Uhakika ni mpaka sasa ni VAR mbili tu, hivyo fursa imepatikana kwa watu kuleta zingine, hasa zile zinazotembea, ili mechi zote nane za Ligi Kuu ziwe na mashine hizo.

Hata hivyo, ushauri wangu ni kuwapo na mafunzo pia kwa waamuzi kwa ajili ya kutoa maamuzi sahihi, kwani uwepo wake pekee haisaidii.

Ninavyojua VAR haitoi maamuzi, ila inamsaidia kumwonyesha mwamuzi yaliyo ili atoe maamuzi yaliyo sahihi, je tumewandaa marefa wetu kwa ajili ya kuitafsiri?

Tunaona katika baadhi ya Ligi za Ulaya, bado makosa ya waamuzi yanaonekana na wanalalamikia. Nadhani wakati VAR zitafanya kazi, kuwepo na mafunzo kwa waamuzi, pamoja na uadilifu kwa sababu wanaweza pia kutafsiri sivyo kwa matakwa yao, kama ilivyoonekana katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Yanga dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Tunataka VAR isaidie waamuzi pale ambapo hawajaona kwa sababu ya kasi ya mchezo, au wamepitiwa, warudie kufanya uamuzi sahihi na siyo ije kuleta utata mwingine wa waamuzi kuanzisha kigugumizi, na kuweka pembeni uamuzi sahihi licha ya mashine huyo kuonyesha wazi tukio.

Kama waamuzi hawatakuwa na mafunzo sahihi, ujasiri, uadilifu na upendeleo, itakuwa kazi bure. Kazi sasa kwa TFF na Bodi ya Ligi kufanya kila kinachowezekana kwa waamuzi, ili VAR iwe kweli mwarobaini wa maamuzi tata.

# Vita mikopo umiza vyatangazwa rasmi

Na Thobias Mwanakatwe

SERIKALI imepaza sauti kwa mikopo umiza kwa kutoa onyo kwa watu binafsi na kampuni zinazojihusisha na utoaji mikopo hiyo kuacha mara moja na watakaoendelea watanyang'anywa leseni.

Jambo hilo, serikali imesema linarudisha nyuma wananchi kiuchumi na kuwaingiza katika lindi la umaskini.

Akiwasilisha mapendekezo ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2024/25 juzi, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema sekta ya fedha imeendelea kukua na watumiaji wa huduma za kifedha wameendelea kuongezeka.

Waziri alisema utafiti uliofanywa na Finscope mwaka 2023 unaonyesha kuwa asilimia 76 ya Watanzania wanatumia huduma rasmi za kifedha ikilinganishwa na asilimia 65 mwaka 2017.

"Pamoja na mafanikio hayo, naielekeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na taasisi zote zinazohusika katika usimamizi wa sekta ya fedha, zikiwamo kamati zote za ulinzi na usalama, kuendelea kufuatilia suala hili kwa ukaribu, kuchukua hatua kali dhidi ya wote wanaotoa huduma za fedha bila kuwa na leseni na kuwanyang'anya leseni wote watakaobainika kuwa wanatoa mikopo bila kuzingatia masharti ya leseni na kuwaumiza wananchi," alisema. Mafanikio hayo, alisema yameleta changamoto mbalimbali katika sekta ya fedha ikiwamo utoaji wa mikopo yenye riba kubwa, maarufu kama mikopo umiza, mikopo kausha damu, mikopo kuzimia na mikopo chuma ulete inayowaumiza wananchi na kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Alisema wako watu wanaowakopesha wakulima kopo la mbegu la kilogramu mbili halafu wanamtaka mkulima atakapovuna alipe gunia la mazao lenye takribani kilogramu 100, sawa na riba ya asilimia 5,000.

"Aidha, wako watu wanaokopeshana fedha kwa makubaliano ya riba ya Sh, 800,000 kwa mwezi ambapo ukikopa Sh. milioni nne utatakiwa urudishe Sh. milioni 28 baada ya miezi 30. Hii ni sawa na riba ya asilimia 240 kwa mwaka. Hii nayo ni dhuluma na ni wizi kama wizi mwingine,"alisema.

Dk. Nchemba alisema viwango hivyo ni vikubwa na vinawarudisha nyuma wananchi na wakati mwingine wanafanya mabadiliko bila kuwa na elimu ya fedha ambapo utaratibu huu ni si huruma bali ni dhuluma na kuiba kwa kutumia matatizo ya Mtanzania.

Aliwakumbusha wananchi kuwa na nidhamu ya fedha ikiwamo kukopa kwa ajili ya mahitaji yenye tija na ikiwezekana kuchukua mikopo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali badala ya matumizi ya kawaida na kuwa makini katika masharti ya mikataba ya mikopo.



Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Prof Abel Makubi (kulia), akipokea vitendea kazi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji anayemaliza muda wake, Dk. Alphonce Chandika, (Kushoto), wakati wakikabidhiana ofisi hospitalini hapo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Muhimbili yahitaji damu chupa 120

Na Christina Mwakangale

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), ina mahitaji ya damu kwa asilimia 37, huku ikihitaji chupa (unit) 120 kila siku, kwa ajili ya huduma hiyo kwa wagonjwa.

Hata hivyo, katika uhalisia wa kinachopatikana kila siku ni chupa 75 na nusu tu, hivyo kuna upungufu wa chupa 44 na nusu.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Shirikishi MNH, Dk. Mbonea Yonazi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Duniani, ifikapo Juni 14 kila mwaka.

Alisema kiwango cha makusanyo ya damu kimeongezeka na kufikia mifuko 5,847 kwa kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 65 kutoka 3,540 mwaka jana.

"Kila Juni 14 dunia huadhimisha siku hii, ili kuweka hamasa kwa jamii. Tunahitaji damu MNH kwa majeruhi wanaopokelewa saa 24, watoto wenye saratani, wajawazito wanaojifungua na wagonjwa wanaosubiri kufanyiwa upasuaji.

"Kila mmoja hayuko salama anaweza kupata tatizo na kuhitaji damu muda wowote. Mifuko 120 tunahitaji kila siku, ingawa kuna ongezeko la makusanyo ikilinganishwa na miezi mitatu ya kwanza mwaka jana," alisema Dk. Yonazi.

Alisema ongezeko hilo linatokana na mchango wa hiari kutoka kwa wadau, taasisi, huku akihimiza shule kuendelea kuchangia damu kutokana na kuwa na kundi kubwa la vijana eneo moja. "Hospitali inakidhi mahitaji kwa asilimia 63, asilimia 37 ni upungufu. Kuna madhara ya kuchelewa kupata damu ni makubwa kwa mgonjwa asipopata damu kwa wakati.

"Kuna gharama Sh. milion 1.5 kila mwaka ili kuhakikisha damu salama na mazao ya damu yanapatikana hapa, kutokana na kuhitaji mifuko ya damu, upimaji.

"Hata kama huna kitu maisha yako yana thamani kwa mtu mwingine hata kama hauna fedha, mali, kwa sababu damu hiyo ukichangia ni thamani kwa mtu mwingine." Dk. Yonazi alisema kuna faida za uchangiaji damu, kwa kufanyiwa vipimo vya awali na mchangiaji kujua hali ya kiafya, kama vile maambukizi homa ya ini B na C, kaswende, kujua kundi la damu, presha, uzito, urefu, wingi wa damu.

"Baada ya vipimo wiki mbili majibu ya damu hutolewa, ukigundulika na shida unaanza matibabu mapema. Hii ni kati ya faida ya kuchangia damu kwa sababu hutumii gharama. Iwapo ungehitaji kupima damu ungelipia zaidi ya Sh. 90,000."

Miongoni mwa wachangia damu, Priscus Kimario, alisema kuchangia damu ndio sadaka ya kipekee kwa waamini wa dini tofauti, ambayo haiangalii uchumi wa kifedha. "Wito umetolewa kwa wenye afya njema kwa sasa, kutoa sadaka ya kuchangia damu, ili kuokoa wahitaji," alisema Dk. Yonazi.

Mkuu wa shule ya sekondari Mivumoni Islamic, Tanu Kamaze, alisema utaratibu wa kuchangia damu ni ibada kama zilivyo zingine, akihimiza jamii, watoto kuchangia damu. Mchangiaji Yahya, mkazi wa Mbezi, mkoani Dar es Salaam, alianza kuchangia damu tangu mwaka 1989 akiwa kidato cha kwanza na hii ni sadaka kwake, akiisihi jamii ifanye hivyo.

# Chanzo kushamiri ukatili chaanikwa

Na Beatrice Shayo

FAMILIA kumaliza kesi za ukatili bila kuchukuliwa hatua za kisheria imeelezwa ni kichocheo cha kuongezeka kwa vitendo hivyo kwa watoto nchini.

Wakizungumza kuelekea maadhimisho ya kimataifa ya siku ya mtoto wa Afrika yaliyoandaliwa na Ubalozi wa Ufaransa, Mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza, Adela Alex, katika Shule ya Precious, alisema migogoro ya ndoa imekuwa ni chanzo cha kuwapo kwa ukatili kwa watoto.

Alisema kitendo cha mzazi kuficha kesi ya ukatili aliofanyiwa mtoto wake ni kushiriki kwenye vitendo hivyo kuendelea kuongezeka.

"Utasikia wazazi wanasema tulimalizana kifamilia au utaharibu jina la familia, lakini hii huchangia ukatili kukua kwa kiwango kikubwa zaidi kwa kuwa hakuna mtu wa kuusemea au itamwaribu mtoto kisaikolojia na kushindwa kuzungumza pale atakapofanyiwa ukatili mwingine anajua hata akisema hatasaidiwa," alisema.

Alisema watoto wanaathirika kiakili na kisaikolojia na wengine kufikia uamuzi wa kujiua kutokana na vitendo vya migogoro vinavyoendelea ndani ya familia.

"Migogoro ya kifamilia inatengeneza tatizo la akili hivi karibuni tumeona mtoto wa miaka 13 amejiua haya yote yanasababishwa na ukatili wa kisaikolojia kutokana na migogoro ya kifamilia hana mtu wa kumuelezea anakata tamaa ya maisha," alisema.

Alex alisema tatizo lingine ni wazazi kutotenga muda kwa ajili ya kuzungumza na watoto wao ili kujua wanayopitia.

Alisema ukatili mwingi unafanyika nyumbani hivyo mzazi anaporudi kumkuta mtoto amelala na wakati mwingine anapotaka kuzungumza juu ya anayopitia mzazi huw mkali.

"Hili nalo ni tatizo kwa mzazi kutokuwa karibu na watoto wao, ni vizuri kujenga urafiki na mtoto wako ili iwe njia rahisi kwake kukueleza yanayomsibu," alisema.

Mratibu wa Dawati la Maendeleo ya Mtoto Manispaa ya Kinondoni, Clara Urasa, alisema wana jukumu la kumwendeleza mtoto katika shughuli zote katika jamii na haki zao kulindwa kupitia majukwaa waliyoyaweka. Urasa alisema watoto wanatakiwa kufundishwa mambo ya msingi ili kuzuia mmomonyoko wa maadili na kumfanya mtoto asimame katika haki zake. Mwenyekiti wa Maandalizi ya Siku ya Mtoto wa Afrika, Agatha Makombe, alisema maadhimisho hayo ni sehemu ya kupaza sauti na kuonyesha utetezi wao kwa watoto.

Alisema wazazi wanatakiwa kushirikiana na watoto hao ili wawe na mienendo mizuri katika jamii na kuepukana na vitendo vya kikatili.

# Kongamano la uwekezaji Lagos kuongeza uwekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC), kimesema mabadiliko makubwa ya kisera na sheria yanayoendelea kufanywa na serikali ya awamu ya sita yamekuwa kivutio kikubwa kwa mitaji kutoka nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Bodi ya TIC, Dk. Binilith Mahenge mjini Lagos, Nigeria wakati wa kongamano la uwekezaji.

Tanzania kwa kushirikiana na Ubalozi wa Nigeria iliandaa kongamano kubwa la uwekezaji nchini humo lengo ikiwa ni kuvutia wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali ndani ya Afrika.

Kongamano hilo ambalo lilifanyika kwenye miji ya Lagos na Enugu lililenga kuwaeleza wawekezaji wa Nigeria fursa mbaliambali za uwekezaji zinazopatikana hapa nchini.

Dk. Mahenge ambaye aliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye kongamano hilo, alielezea mageuzi makubwa ambayo Rais wa awamu ya sita, Samia Suluhu Hassan ameyafanya na kuvutia uwekezaji kutoka nje.

Alisema Tanzania imefanya mageuzi makubwa kwenye sheria na kanuni zinazosimamia uwekezaji na imeweka na vivutio mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na wale wa kigeni.

"Katika kukuza diplomasia ya uchumi serikali ya Tanzania imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na hali hiyo imewavutia wawekezaji wengi kutoka mataifa mbalimbali," alisema Dk. Mahenge.

Alisema kwenye kongamano hilo ujumbe wa (TIC) ulifanya vikao na wenzao wa Chemba ya Biashara na Viwanda Lagos na walikutana pia na Chemba ya Biashara, Viwanda, Madini na Kilimo ya mji wa Enugu (ECCIMA).

Alisema kwenye kongamano hilo raia wengi wa Nigeria waliohudhuria walielezea kufurahishwa na fursa mbalimbali za uwekezaji zilizoko nchini na kuahidi kuja kutafuta wabia wa sekta binafsi.

Kongamano hilo lilijadili kuhusu sekta ya uzalishaji viwandani, ujenzi wa majengo, utalii, dawa, uchumi wa buluu, misitu, mifugo, huduma za kifedha, mafuta na gesi na uchakataji wa mazao ya chakula.



Mmoja wa washiriki akichangia mjadala wakati wa kongamano la uwekezaji lililoandaliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania, jijini Lagos, nchini Nigeria, hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Akiba fedha za kigeni yafikia Dola bil.5.3

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imesema hadi kufikia Machi mwaka huu akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Marekani bilioni 5.3, kiasi ambacho kinakidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi minne.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema hayo juzi bungeni wakati akiwasilisha mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/25.

Dk. Nchemba alisema kiasi hicho ni juu ya lengo la nchi la muda usiopungua miezi minne.

Alisema serikali iliendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza nakisi ya urari wa biashara uliopelekea kupungua kwa nakisi hiyo kutoka Dola za Marekani bilioni 5.3 mwaka 2022 hadi Dola za Marekani bilioni 2.7 kwa mwaka ulioishia Februari 2024 kwa kuongeza mauzo nje na kupunguza uagizaji wa bidhaa zinazozalishwa nchini.

"Sisi Watanzania pia tunalikuza tatizo la upungufu wa dola kwa baadhi ya watu kudai malipo au kufanya malipo ya bidhaa na huduma zinazotolewa ndani ya nchi kwa kutumia fedha za kigeni yaani, dollarization," alisema.

"Taasisi ipo Tanzania na pengine hata taasisi ya serikali, inamuuzia huduma mtanzania inamwambia alipe kwa dola, taasisi zingine zinataka mtanzania alipe ada kwa dola, alipe kodi ya nyumba kwa dola, vibali vya kazi, leseni na kadhalika kwa dola. Tunawafanya watanzania wahangaike kuitafuta fedha ya kigeni kununua huduma zinazotolewa ndani ya nchi yao," aliongeza.

Alisema jambo hilo linasababisha kuongezeka kwa mahitaji yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni na kuwanyima fursa watu wanaohitaji fedha za kigeni kwa ajili ya kulipia bidhaa na huduma muhimu kutoka nje ya nchi.

Dk. Nchemba alisema kitendo cha kuuza bidhaa au huduma za ndani kwa kutumia fedha za kigeni ni kosa kwa mujibu wa Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 2006, ambacho kinabainisha kwamba shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali pekee kwa malipo ya ndani ya nchi.

Kutokana na hali hiyo, Waziri aliwataka wadau wa ndani, taasisi za umma, wafanyabiashara, asasi za kiraia, mashirika ya kimataifa na watu wote waliopo nchini wenye tabia ya kuweka bei kwenye huduma au kuuza bidhaa kwa fedha za kigeni kuacha mara moja na kuhakikisha bei za bidhaa na huduma hizo zinatangazwa na kulipwa kwa shilingi ya Tanzania.

Pia aliziagiza taasisi zote za serikali zinazotoza ushuru, ada na tozo mbalimbali kwa fedha za kigeni kurekebisha kanuni zao ili tozo hizo zilipwe kwa shilingi.

"Hata mgeni akija na fedha za kigeni ni vyema akaibadilisha kuwa fedha ya kitanzania ili aweze kupata huduma.

Tunafanya kila malipo kwa fedha za kigeni, halafu Shilingi ikishuka thamani tunajiuliza tumekosea wapi." Alisema.

## Halmashauri zakumbushwa bajeti ya watu wenye ualbino

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HALMASHAURI nchini zimeshauriwa kutenga bajeti kwa ajili ya kununua mafuta ya watu wenye Ualbino kuwaondolea kikwazo cha kuyapata kwa urahisi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema hayo juzi wakati akimwakilisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana , Ajira na Watu wenye Ulemavu, Deogratias Ndejembi, kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuongeza Uelewa kwa Watu Wenye Ualbino.

Maadhimisho hayo ambayo yalifanyika Mailimoja, Kibaha yalijumuisha watu wenye ualbino kutoka maeneo mbalimbali nchini ambao waliendelea kutoa elimu ya uelewa kwa jamii kuhusu masuala ya wenye ualbino.

Kunenge alisema halmashauri zinatakiwa kuzingatia maagizo hayo ya kutenga fedha za mafuta kwani suala hilo lina uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya watu wenye ualbino.

Aidha, Kunenge alisema katika uoaji wa fedha za vikundi, watu wenye ualbino wanapopeleka maombi ya kupata vyerehani, wanunuliwe vyenye ubora ambavyo vitakidhi makusudio yao.

Mkuu huyo wa Mkoa alipongeza jitihada za serikali kutengeneza mafuta ya watu wenye Ualbino jambo ambalo ni hatua kubwa na kwamba maboresho yanaendelea kukidhi mahitaji ya walengwa hapa nchini.

Kadhalika, Kunenge alisema kwa sasa serikali inaendelea kuhakikisha elimu ya uelewa kuhusu wenye ualbino inafika kwa jamii, huku maelekezo yakitolewa kwa maofisa ustawi wa jamii na maofisa elimu kuwatambua watu wenye ualbino. Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Raphael Meela, alisema serikali inahakikisha usalama umeimarishwa kwa watu wenye Ualbino.

Alisema zaidi ya polisi kata 3,000 wamesambazwa kila mkoa, hivyo hakuna haja ya kuwa na hofu ya usalama wao kwenye maeneo yote wanayofanyia shughuli zao.

Mwenyekiti wa Chama Cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), Godson Mollel, aliomba serikali kuingilia kati kutokana na kuchoka na vitendo vya ukatili vinavyofanywa kwa kundi hilo.



# 'Jihadharini wanasiasa wenye lugha chochezi'

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata, amewataka wananchi kuwakataa viongozi wa kisiasa wanaotoa kauli za kichochezi, kibaguzi na zenye viashiria vya kuvunja amani nchini.

Akizungumza juzi na wananchi mjini Kiomboi wilayani Iramba kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa Stendi ya mabasi alisema wapuuze maneno yanayosemwa kwa lengo la kutaka kuwapotosha na kuwadanganya watu.

Mlata alisema wananchi waendelee kumuombea na kumuamini Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambae amejitoa kuwaletea maendeleo katika sekta ya maji, afya,umeme, barabara na elimu.

Alisema adha ya usafiri waliyokuwa wakiipata wananchi huko nyuma, ambapo walilazimika kutoka Iramba kwenda kupanda gari Singida mjini kuelekea Dar es Salaam, lakini leo hii mabasi yanaanzia safari mjini Kiomboi kwa sababu ya uwepo wa barabara nzuri za lami.

Mlata alisema wanafunzi walilazimika kutumia vibatari wakati wa kujisomea ambavyo viliingiza moshi puani hali ambayo hivi sasa haipo kwa sababu Rais Dk. Samia amefikisha umeme katika vijiji vyote, hivyo wanakila sababu ya kuendelea kumuunga mkono.

Kuhusu elimu ameeleza watu walikua wanafaulu lakini anayepata bahati ya kuendelea na masomo anachaguliwa mmoja tu lakini hivi sasa shule zimejengwa katika kila kata kwa kutumia zana za kisasa.

Akizungumzia kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, alisema ni tunu ya Taifa, wazee wao waliungana kwa sababu walikua wanataka kuleta maendeleo.

"Viongozi wangu wa dini niwaombe muendelee kumuombea Rais wetu na kumtaka anayejiita mchungaji anayetamka kuwa Rais amekataliwa na Mungu akatubie kwa kuwa yeye ndio amekataliwa na Mungu kwa kukosa weledi wa kuhutubia," alisema.

Katibu wa CCM Mkoa wa Singida, Lucy Boniface, alisema haikubaliki kwa kiongozi wa chama cha sisasa kuomba kibali cha kuhamasisha na kuimarisha chama chake halafu akishapanda katika jukwaa anahubiri habari ya kuvunja Muungano.

Alisema Hayati Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema atakae anza kusema sisi watanganyika na wao wazanzibari laana itamtafuna ndio maana chama cha kiongozi huyo kinatafunwa kwa sababu ya kutaka kuwarudisha Watanzania kwenye ukabila na ubaguzi wa kidini.

# Mavunde atangaza timu ya dira madini

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ametangaza timu ya wataalamu ya kuandaa andiko maalum linalobeba maudhui ya Maono 2030 (Vision 2030) kwa sekta ya madini huku akiipa kibarua kizito cha kutilia mkazo maeneo nane yenye tija kwa Watanzania.

Akizungumza jana kwenye hafla ya kuzindua timu hiyo jijini hapa, Mavunde alisema timu hiyo itasaidia kuandaa ramani ya sekta ya madini kwa miaka michache ijayo ili ifikapo 2030, asilimia 50 ya eneo la Tanzania liwe limefanyiwa utafiti wa kina.

"Tunataka tuwaongoze vizuri watanzania kupitia sekta ya madini wakapate taarifa sahihi ya kilichomo chini ya ardhi ili kusaidia kukuza uchumi wetu, tukimaliza utafiti tutapata taarifa za Kijiolojia, ili wawekezaji waone maeneo ya kuwekeza," alisema.

Alisema dira hiyo ni mikakati ya wizara ilivyojipanga kutekeleza maono hayo yanayotokana na maelekezo ya Rais aliyoyatoa katika Mkoa wa Lindi ambapo alielekeza Wizara kuhakikisha inaboresha eneo la utafiti wa kina ili watanzania wasiendelee kuchimba kwa kubahatisha.

"Baada ya maelekezo ya Rais (Samia Suluhu Hassan), wizara tulikaa na kuja na 'Vision 2030 Madini ni Maisha na Utajiri', kwa nini 2030? Nchi yetu imejaliwa kuwa na madini ya aina mbalimbali lakini hatuna uwezo mkubwa wa kubaini kiwango cha madini tuliyo nayo chini ya ardhi. Tunataka mwaka 2030 tuwe tumefikia asilimia 50 ya eneo la Tanzania liwe limefanyiwa utafiti wa kina," alisema.

Alisema Tanzania ina ukubwa wa kilomita za mraba 945,000 na eneo lililofanyiwa utafiti wa kina wa Madini nchini ni asilimia 16.

"Katika eneo hili lililofanyiwa utafiti tumefanikiwa kwa Mwaka 2023/24 sekta ya madini imeongoza kwa mchango mkubwa wa kuiingizia nchi fedha za kigeni, asilimia 56 ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi, fedha zilizopatikana zinatokana na sekta hii ya madini, tulifanya mauzo ya bidhaa nje ya nchi zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.1," alisema.

Alibainisha kuwa timu hiyo itakabidhiwa hadidu za rejea 14 zitakazowaongoza kuandaa ramani ya utekelezaji wa maono hayo.

"Timu hii inayoongozwa na Prof. Mruma tumekabidhi sekta hii mikononi mwenu, mna nafasi ya kuleta mageuzi chanya au kuifanya Tanzania ipotee kwenye ramani, mna nafasi ya kutuonesha sekta hii ya madini na mchango wake ili watanzania wanufaike na rasilimali hii ambayo tumejaliwa," alisema.

Alitaja maeneo ya kuzingatiwa kwenye uandaaji wa andiko hilo ni mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa unaongezeka, upatikanaji wa fedha za kigeni, maendeleo ya viwanda na sekta mbalimbali, ushiriki wa watanzania kwenye sekta ya madini.

"Shirika letu la madini (STAMICO) tunataka kulifanya liwe shirika kiongozi. Nataka watu waje waombe kazi ya kuchoronga kwenye migodi yake na sio kwenda kuomba kazi ya kuchoronga kwenye migodi ya watu," alisema.

Pia alisema anatarajia andiko hilo litakuwa mwarobaini wa migogoro ya wachimbaji wakubwa na wadogo na kuvutia uwekezaji nchini.

Naye Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Kamishna wa Madini, Dk. Abdulrahman Mwanga, alisema watahakikisha wanasimamia maono hayo ili kuleta mafanikio yaliyokusudiwa.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Dk. David Mathayo, alipongeza wizara kwa hatua hiyo kwa kuwa ni mwarobaini wa kukuza uchumi wa nchi kupitia madini.



Waziri Mkuu mstaafu, Dk John Malecela akizugumza wakati akifungua kongamano la vijana katika uwanja wa Kanisa la Revival Evangelist Assemblies of God Tanzania Mtera, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Malecela awafunda vijana matumizi fursa

**Na Peter Mkwavila,**
MPWAPWA

WAZIRI Mkuu na Makamu wa kwanza wa Rais Mstaafu, John Malecela, amesema vijana nchini wanapaswa kuzitumia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali badala ya kukaa vijiweni na kulalamika kukosa kazi ya kufanya.

Malecela pia amewataka vijana kuibua miradi na kuunda vikundi vitakavyo wawezesha kupata mikopo ambayo inatolewa na halmashauri ikiwemo ile ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema hayo juzi alipokuwa akifungua kongamano maalumu la maombi lililoandaliwa na vijana wa Kanisa la Revival Evangelist Assemblies of God Tanzania Jimbo la Dodoma, Mtera wilayani Mpwapwa.

Alisema serikali ya awamu ya sita imewekeza fursa mbalimbali kinachotakiwa ni vijana kuungana na kubuni miradi ambayo itawawezesha kupatiwa mikopo na halmashauri.

"Niwaombe vijana wa hapa Mtera ambao mmebahatika kuwa na bwawa tumieni fursa ya bwawa hili kwa kuunda vikundi ili muombe mikopo ambayo itawapelekea kupata fedha ambazo mtawekeza kwenye sekta ya uvuvi na kilimo cha bustani," alisema.

Pia aliwataka vijana kujiamini na kuondokana na hofu ya kushindwa maisha bali watumie ujana wao kwa kutochagua kazi ikizingatiwa kuwa umasikini hauwezi kuondoka bila kufanya kazi zilizo halali na zinazoweza kuwainua kiuchumi.

Malecela pia aliwaomba kwenye kongamano hilo la maombi kutumia nafasi zao kama vijana kuiombea serikali pamoja na uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika nchini kote mwaka huu pamoja na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Alisema pamoja na maombi hayo ya kuombea uchaguzi huo vijana hao wametakiwa kujitokeza kwenda kujiandikisha katika daftari la mpigakura na kugombea nafasi hizo za uenyeviti wa serikali za mitaa.

Awali, akizungumza kwenye kongamano hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Taifa, Askofu Mstaafu Jackson Madelemo, aliwataka vijana kuishi na jamii kwa utii huku wakiunga mkono jitihada za serikali katika kuleta maendeleo.

Hamsa Simwinga, akisoma risala ya vijana alisema watatumia kongamano hilo kufanya maombi maalum kwa ajili ya uchaguzi, kuwaombea Rais na wasaidizi wake.

Alisema vijana wanatambua mwaka 2024 na mwaka ujao wa 2025 nchi inakabiliwa na jukumu zito la uchaguzi hivyo watatumia fursa hiyo ya kongamano kuombea uchaguzi huo ili ufanyike kwa haki na amani na Mungu kuwapa viongozi walioandaliwa na yeye mwenyewe.

## SMZ yaelekeza nguvu ujenzi wa uwanja wa ndege

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali ya Zanzibar imeweka mpango wa kujenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa kisiwani Pemba utakaoruhusu ndege kubwa kutua kisiwani humo ili kikifungua kisiwa hicho kiuchumi na kukuza sekta ya utalii.

Pia amesema Zanzibar ina azma ya kuzifungua barabara kubwa zenye hadhi ya juu kutoka Wete hadi Chake na kutoka Chake hadi Mkoani mwishoni mwa mwaka huu ili kukikuza kisiwa cha Pemba kibiashara na uwekezaji.

Dk Mwinyi aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa hotel ya The Mora uliofanyika juzi Matemwe, mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema tayari serikali imetia saini mkataba wa ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Pemba ili ndege za kimataifa zitue kisiwani humo.

Kuhusu maboresho makubwa ya uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume, Dk. Mwinyi alisema baada ya kukamilika kwa hatua kubwa ya jengo namba tatu ambalo kwa sasa linafanya vizuri kimataifa, serikali pia inafanya matengenezo makubwa kwa jengo la kwanza na la pili la abiria na ujenzi mpya wa jengo la nne ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na utalii nchini.

Pia alitaja faida za uwekezaji zimechangia asilimia kubwa ya maendeleo ya nchi kutokana na kodi wanazolipa wawekezaji kwa serikali ambazo hutumiwa kuboresha huduma za jamii ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara na mawasiliano, ujenzi wa shule mpya, hospitali, masoko na kusambazwa kwa maji safi na salama.

Dk. Mwinyi pia alisema uwekezaji unafungua fursa nyingi kwa wazawa wakiwamo wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara kupata soko la uhakika la bidhaa zao kupitia hoteli mbalimbali.

Alisema serikali huwalazimisha wawekezaji kuboresha huduma za jamii maeneo yote yaliyopitiwa na uwekezaji ikiwamo kujenga vituo vya afya, ujenzi wa vituo vya watoto yatima pamoja na mahitaji husika ya maeneo hayo.

Rais Dk. Mwinyi alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif, kuwasimamia wawekezaji wote kununua mahitaji yote yanayozalishwa nchini kabla ya kuagiza nje ya nchi ili kutanua fursa kwa wajasiriamali wazawa na wafanyabiashara wa ndani.

Akisifia uzuri na haiba ya kisiwa cha Zanzibar, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Tui Group inayomiliki hoteli ya The Mora, Sebastian Abel, alisema Zanzibar ni kisiwa chenye hadithi nyingi nzuri zenye kumvutia kila mgeni anayetembelea na ni zawadi na sehemu salama ya uwekezaji na biashara ndio maana wamevutiwa na kuwekeza nchini.

Waziri Sharif aliwahakikishia ushirikiano wa hali ya juu wawekezaji wote walioko Zanzibar na kusisitiza kuwa maendeleo makubwa kwenye sekta ya uwekezaji ni juhudi za Rais Mwinyi.

Mkurugenzi Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Saleh Saad Mohamed, alisema hoteli ya The Mora yenye hadhi ya nyota tano inamilikiwa na kampuni ya Tui Group ambayo tayari imewekeza nchini zaidi ya Dola za Marekani milioni 500 kwenye sekta ya utalii kupitia hoteli zake za RIU iliyoko Nungwi, TUI BLUE ya Mangapwani na The Mora.

# Waziri Mkuya aeleza umuhimu mfuko TIMIZA

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (TIMIZA FUND) utaisaidia serikali kuwashirikisha wananchi wake katika uwekezaji na shughuli za kiuchumi kwa lengo la kuboresha kipato cha kuendesha maisha yao.

Aliyasema hayo jana katika hotuba yake iliyosomwa na Naibu Waziri wake, Juma Makungu wakati wa uzinduzi wa mfuko huo hafla iliyofanyika visiwani hapa.

Alisema mfuko huo utatoa fursa kwa wananchi wa kipato cha chini kushiriki katika uchumi na kuongeza kiwango cha utumiaji wa fedha na uchumi jumuishi.

Mkuya alisema uongozi wa TIMIZA FUND na wadau wanapaswa kuyafanyia kazi mambo yote waliyoahidi katika waraka wa toleo la mfuko huo ili kuendelea kujenga imani kwa wananchi. "Usimamizi wenye weledi na uadilifu wa TIMIZA FUND unategemewa katika kuleta maendeleo makubwa zaidi, hivyo sote tunaojihusisha na sekta hii, twendeni tukayafanye tunayoyasema kwa mujibu wa sheria na kanunui zinazotuongoza" alisema Makungu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Zan Securties, Raphael Masumbuko, alisema mfuko wa uwekezaji wa pamoja utasaidia kufungua milango ya fursa mbalimbali hata zile zilizopo nje ya uwezo wa mtu mmoja mmoja na uwekezaji huo ni kwa watu wote wa vipato vya aina zote.

Mwenyekiti wa Bodi ya Zan Security, Abdulsalaam Issa Khatib, alisema mfuko huo ni chachu ya kuleta mabadiliko ya tamaduni na hamasa za wawekezaji kuweka akiba ili kuleta ushindani wa mifuko na kuleta tija kwa mifuko na Taifa kwa ujumla.

Aidha, alisema jambo hilo ni la kihistoria katika sekta ya uwekezaji kutokana na umuhimu wa masoko na mitaji ya Zanzibar na kuitaka Serikali kushauri taasisi za umma kuwekeza katika sekta ya mitaji na kujiorodhesha katika soko la hisa ili kutoa hamasa kwa mifuko ya uwekezaji.

Akizungumza kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam, Emanuel Nyalali ameishukuru serikali kwa kuanzisha sera na kanuni zinazowezesha sekta za masoko na mitaji kukuwa nchini. Aliwataka wafanyakazi kuwekeza katika mfuko huo ili kutimiza malengo waliyojipangia ikiwamo kuwekeza kwa ajili ya mahitaji ya elimu, ujenzi,ukarabati wa nyumba, kustaafu,, gharama za safari za likizo, pamoja na huduma za afya.

Mfuko wa uwekezaji wa pamoja umeanzishwa mwaka 2019 chini ya Zan Securties kwa lengo la kuwashirikisha wananchi kujiunga na mfumo wa masoko ya mitaji na dhamana ili kunufaika kiuchumi.




Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya wachangiaji damu katika makao makuu ya damu Salama, Sebleni Wilaya ya Mjini juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaweka wazi hali ya damu salama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema Zanzibar haina uhaba wa damu lakini pia haina damu ya kutosha ambayo imehifadhiwa katika benki ya damu kama ni damu ya akiba.

Akizungumza kuhusu maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Duniani ambayo hufanyika Juni 14 kila mwaka, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kuchangia damu ili kuokoa maisha ya watu wanaohitaji huduma hiyo,

Alisema sababu kubwa zinazopelekea kuhitaji tiba ya damu ni kupoteza damu kwa wingi hasa wakati wa kujifungua, ajali au tiba ya upasuaji na pia upungufu wa damu kwa watoto chini ya miaka mitano wenye kuugua maradhi ya mifupa na watu wazima kutokana na sababu mbalimbali.

Mazrui alisema Mpango wa Taifa wa Damu Salama ambao unazingatia uchangiaji wa damu kwa hiari, ulianza mwaka 2005 Zanzibar chini ya Wizara ya Afya kwa ufadhili mkubwa wa Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupunguza Kasi za Maambukizi ya UKIMWI (PEPFAR).

"Nia ni kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI na pia kuziwezesha hospitali kuwa na akiba ya damu ya kutosha wakati wote kwa ajili ya matumizi na si kusubiri mpaka dharura itokee kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo damu zilikawia kufika wagonjwa wahitaji na kusababisha wengi wao kupoteza maisha," alisema.

Waziri alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24 mpango umejiwekea malengo ya kukusanya chupa za damu 20,000 na hadi kufikia Machi, mwaka huu, mpango ulikusanya chupa 16,155 sawa na asilimia 80.8 kwa Zanzibar.

Alisema maombi ya damu yaliyopokewa kutoka hospitali zinazotoa tiba ya damu ni 38,595 na kufanikiwa kusambaza 19,785 sawa na asilimia 51 ya maombi hayo.

Kila mmoja, alisema ni muhitaji wa damu, hivyo ni vyema kuweka akiba kabla ya kusubiri dharura kutokea na kuwataka wachangiaji damu kuendelea kuchangia ili kuhakikisha benki hiyo inakuwa na damu ya kutosha na kukidhi mahitaji .

Aidha, Waziri Mazrui alisema elimu ya lishe inahitajika kwa jamii kwa sababu kuna changamoto kubwa ya wananchi wa Zanzibar kuwa na lishe duni na bila lishe nzuri lengo la uchagiaji wa damu halitafikiwa.

Alisema mahitaji ya damu ni makubwa Zanzibar na katika miaka 20 ya kuanzishwa kwa benki ya damu na uchangiaji wa damu mwaka 2021/22 benki hiyo ilivunja rekodi kwa kukusanya damu nyingi na kuvuka malengo ambapo ilikusanya chupa 20,000 wakati lengo lilikuwa chupa 16,000.



NDARO
UKURASA 12



# HIZO MBWEMBWE TU...

MUZIKI wa Bongo Fleva unazidi kuwa maarufu Afrika Mashariki na duniani kote, kutokana na kupambwa na mbwembwe mbalimbali kutoka kwa wasanii.

Kuna baadhi ya wadau wanasema kama kusingekuwepo na mbwembwe nyingi zilizoambatana na mabifu kwa wasanii, basi Bongo Fleva isingekuwepo katika nafasi iliyopo sasa.

Katika mwendelezo wa kunogesha, mashabiki wa muziki wanasubiri ngoma iliyowashirikisha wanamuziki maarufu Harmonize na Rayvanny, wakitaka kuona kama itaweza kuwateka.

Mbwembwe za wasanii hao wawili kwa muda wa wiki tatu sasa zimekuwa zikiwavutia watu wengi, hasa kutokana na wote wawili kutoka katika lebo moja ya WCB na kisha kujiengua.

Kabla ngoma hiyo hajatambulishwa rasmi, tayari mashabiki wameanza kutoa maoni tofauti kuhusu kolabo ya wanamuziki hao, huku idadi kubwa wakiamini itakuwa kali na kuzipita nyimbo nyingine za wasanii wakubwa hapa nchini walizozitoa hivi karibuni.

Hata hivyo, baadhi ya wadau wa muziki wamesema Harmonize na Rayvanny wana vipaji vya kipekee, lakini wanaweza kushindwa kufikia lengo kama watataka kuwapita wengine badala ya kuangalia mashabiki wanapenda nini kutoka kwao.





BASI SAWA

## Daz Baba anakuonya 'Mlinde'



MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, Daz Baba, amerudi tena kuwaburudisha mashabiki wake baada ya kutambulisha ngoma yake mpya inayoitwa 'Mlinde' ambayo inafanya vizuri katika majukwaa ya muziki.

Akizungumza na BT, Daz Baba amesema ngoma hiyo ambayo ina miondoko ya Reggae ameitoa kwa mfumo wa audio, wakati maandalizi ya video yake yatakamilika hivi karibuni.

"Nimerudi katika gemu kwa ladha tofauti, nataka mashabiki zangu watambue ukimya wangu haukuwa bure kwani nilikuwa jikoni napika ngoma ambayo itawaburudisha na kuwapa mafundisho," amesema Daz Baba.

## Cheni ya Idris gumzo mitaani



Mkufu anaovaa mwigizaji, na mshindi wa Big Brother Afrika, 2014, umezua gumzo mitaani na mitandaoni, kila mmoja akiongea lake.

Mitaani na mitandaoni kumechafuka kutokana na aina ya mkufu wa gharama anaovaa, wengine wakidai si bure kutoknana na gharama yake kuwa kubwa, huku wakidai wanavyomfahamu hana uwezo wa kuununua, wengine wakimtetea na kudai ana uwezo wa kufanya hivyo.

"Vijana wanaoamini kuwa utajiri, mafanikio ya mtu yanaletwa na imani za kishirikina au wale jamaa wanaofanya watu kupata pesa, wana akili za kimasikini ni ngumu sana kufanikiwa kimaisha," alisema mchangiaji mmoja.



# CHINO AMPA TAFU MAVOKO

Siku si nyingi mashabiki wa muziki wa bongo fleva watapatiwa zawadi ya ngoma kali kutoka kwa Rich Mavoko, akimshirikisha mshikaji wake mkubwa, Chino wana Man.

Ngoma hii imetajwa ni maalum kwa ajili ya kumrudisha Mavoko kwenye chati, kwani amepitia wakati mgumu kimuziki tangu alipoondoka WCB.

Kutokana na hilo, inaelezwa, Chino ambaye kwa sasa yupo juu, amepanga kumrudisha rafiki yake mkubwa kwenye chati, kwa kuweka voko katika ngoma yake mpya anayotarajiwa kuitoa.

Kama Mavoko alivyomtoa Chino wana Man wakati bado hajulikana inawezekana ngoma hiyo, ikamrudisha Mavoko kwenye chati.





# Komedi tishio kwa bongo fleva

Mashabiki wa burudani nchini wameonya kuwa vipindi vya vichekesho kwenye televisheni mbalimbali nchini kwa sasa vimeanza kuteka hisia za watu, wakiwaonya wasanii wa bongo fleva kuwa makini kwani wanaweza kushushwa kibiashara wasipojiangalia.

Uzi unaoendelea kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii, inayuhusu mambo ya burudani, unasema hata wasanii wa komedi kwa sasa wameanza kuwa maarufu kiasi cha kuwa sawa na wasanii wa bongo fleva, hivyo kuwataka wajikite kwenye malumbano, badala yake wafanye kazi ili kuendelea kuwa juu.

Mashabiki ambao walionekana kuwapa maua yao, wasanii Ndaro na Leonardo, wamesema kwa siku za karibuni wasanii wa vichekesho wamekuwa wakifanya maonyesho ya jukwaani na watu wamekuwa wakijaa, wakati mwingine kuliko hata muziki wa bongo fleva kitu ambacho ni hatari kwa mustakabali wa muziki huo.

"Ukweli kwa sasa komedi imeonekana kuwa na nguvu na ushawishi mkubwa sana na imekaa kibiashara zaidi ukilinganisha na muziki," alisema Tabia Hassan.

## BONGO MUVI WA 5 WALIOFARIKI GHAFLA

**Na Adam Fungamwango**

BINADAMU ana nyakati za furaha, na huzuni pia. Nyakati za huzuni ni pale wanapopoteza kitu chake chochote kinachompa furaha, faraja na amani. Ndiyo maana si lazima afiwe na ndugu yake wa damu, bali yoyote yule anayemhusu, kama vile ukoo, jirani, au anayemfahamu.

Ndiyo maana Watanzania hupitia kwenye wakati mgumu wanapofiwa na watu maarufu, kama wanamuziki, wanamichezo, viongozi, wanasiasa na wasanii.

Hali inakuwa mbaya zaidi wanapofariki ghafla, kwa ajali, au magonjwa yanayosababisha vifo vya aina hiyo.

Tutakuwa na mlolongo wa vifo vya wanamuziki na wasanii, lakini leo tutawaangalia waigizaji, au wasanii wa bongo muvi, ambao walifariki ghafla na kuacha majonzi, wakiliza mashabiki wengi nchini.

**1-Stephen Kanumba-2012**

Ndiye msanii aliyefariki, akaumiza, kuliza mashabiki wengi, msiba wake ulihudhuriwa na umati mkubwa wa watu zaidi mpaka sasa kuliko mwingine yoyote nchini.

Ilikuwa ni ngumu zaidi hata kushika gari lililobeba mwili wake. Msanii huyu nguli wa bongo movie, aliyekonga nyoyo za mashabiki wengi kwa filamu zake kali, alifariki dunia ghafla Aprili 7, 2012 jijini Dar es Salaam, baada ya ubongo wake kupata hitilafu aliposukumwa na msichana aliyedaiwa kuwa ni mpenzi wake.

**2-Sharo Milionea-2012**

Ni mmoja kati ya wasanii wa kuigiza ambaye ndiyo kwanza alikuwa anakuja juu kwenye tasnia ya uigizaji nchini.

Alikuwa na staili ya pekee aliyojichagulia.

Kwa muda mfupi tu, akaondokea kupendwa na vijana wengi, lakini ajali ya gari aina ya Toyota Harrier ilikatisha maisha yake, Novemba 26, 2012, eneo la Maguzonizoga wilayani Muheza, akitokea Dar es Salaam, kuelekea Muheza kwa ajili ya kuwasalimia wazazi wake. Jina lake kamili aliitwa, Hussein Ramadhani.

**3. Rachel Haule-2014**

Huyu ni staa mwingine bongo movie aliyefariki ghafla na kuacha simanzi kwa mashabiki wake na tasnia nzima ya bongo muvi.

Alifariki Mei 2014 jijini Dar es Salaam, ghafla kutokana na tatizo la uzazi, ambapo alifanyiwa upasuaji ambao haukufanikiwa na akaaga dunia yeye na kachanga kake.

Alifariki wakati akiwa ameanza kuwa tishio kwa waigizaji wa kike nchini na kuanza kujichukulia umaarufu mkubwa.

**4. Kinyambe-2016**

Ilikuwa ni Mei 2016, mashabiki wa muvi za Kibongo na vichekesho, walipopatwa na mshtuko, walipopata habari za kufariki kwa muigizaji wa filamu na mchekeshaji Mohammed Abdallah, maarufu kama Kinyambe katika hospitali ya rufaa ya Mbeya, baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Alifariki akiwa anaelekea kwenye kilele cha mafanikio ya kazi yake, kwani muda mfupi tu alikuwa amejizolea mashabiki wengi kutokana na staili yake ya pekee aliyochagua kuiwasilisha kwenye hadhira, iliyowaacha wengi wakiwa hoi kwa vicheko.

**5-Mzee Jengua-2020**



Msanii mkongwe, Mohamed Fungafunga, maarufu kama mzee Jengua, alifariki dunia ghafla Desemba 2020, Mkuranga mkoani Pwani, baada ya kupata tatizo la shinikizo la moyo.

Kifo chake kilileta simanzi kwani pamoja na ukongwe wake, lakini alikuwa mashabiki walikuwa wanamhitaji kutokana na aina yake ya uigizaji walioipenda, akiigiza mzazi mkali au mtu mwenye misimamo isiyoyumba, mwenye uwezo wa kutetea jambo lolote lile mbele ya jamii bila woga, hata kama amekosea na ni yeye peke yake anayelipigania.

FILAMU

# Denti : Wapiganapo mafahari, nyasi zinaumia




**Na Adam Fungamwango**

WAGOMBANAPO mafahari wawili ziumiazo ni nyasi. Huu ni msemo wa Kiswahili wenye maana kuwa wanapogombana watu ambao wana uwezo unaofanana, basi wale walio chini yao ndiyo watakaoathirika.

Mtunzi wa filamu ya 'Denti' amejaribu kuliangalia hili ndani ya jamii na kuja na kitu kama hiki kwa ajili ya kuelimisha.

Waliocheza filamu hii ni Blandina Chagula aliyecheza kama mke wa Deo, Slim Omari ambaye ndiye Deo mwenyewe, Gladyness Steve aliyecheza kama Linda, Afsa Omari Thageo Alexander na wengineo, ambao kwa kiasi kikubwa inaonyesha wanapogombana wazazi, ni watoto ndiyo wanaoumia.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa Deo na mkewe wakigombana kiasi cha kupigana. Binti yao Linda anashuhudia ndondi hizo, anaonekana kuumizwa mno na tabia ya wazazi wake ambao kila kukicha wao ni kubishana, ugomvi na ngumi.

Mawazo kichwani yanamfanya hadi kutofanya vema darasani. Walimu wanashangaa, alikuwa denti mwenye akili nyingi awali.

Linda analieleza tatizo la wazazi wake kwa rafiki yake wa jirani. Hakuwa rafiki mwema, kwani anamshauri kujisahaulisha mambo hayo kwa kunywa pombe, na anasa. Anakataa kufanya hivyo. Lakini kila kukicha ni afadhali ya jana. Mwisho anaungana na rafiki yake. Linda anabadilika tabia.

Anaanza kunywa pombe, kuvuta sigara na ngono zembe.

Siku moja anaamua kwenda anakokutana na rafiki zake, lakini hawakuti. Anajaribu kwenda kijiwe kingine anakutana na mvulana anayemtongoza ili kufanya naye mapenzi. Akakubali, lakini wakati wanaingia chumbani tu, anakutana na wavulana wengine wawili ambao wote wanambaka.

Kisa hicho kinamfanya kukacha kabisa shule. Kama kawaida wazazi wa Linda wanaanza kugombana kutokana na kubadilika kwa tabia ya binti yao kila mmoja akimtuhumu mwenzake.

Walimu wake wanaamua kumsaka kwa sababu hafiki shule na nyumbani hakai sana. Wanamfuma kwa mpenzi wake akiwa hajiwezi kwa kutumia madawa ya kulevya.

Walimu wanamchukua na kumpeleka hospitalini ili apate matibabu. Wanawasiliana na wazazi wake, lakini wanapokutana hospitalini kazi ni ile ile tu, ugomvi.

Walimu wanawaamua na kuwakalisha chini wakiwaambia ili kuokoa maisha ya mtoto wao, wasiendelee na tabia aliyonayo, ni wao kuyamaliza yote na kuishi kwa amani nyumbani, vinginevyo wanampoteza mtoto wao. Wakaahidi kubadilika tabia mbele ya walimu wa binti yao.



## Kanye kweli hujabadilika

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West na mpenzi wake Bianca Censori, wamekuwa kivutio nchini Japana kutokana vitendo vyao vilivyojaa utata.

Kulingana na mtandao wa TMZ, wawili hao walitumia muda mwingi katika mgahawa wa uitwao Il Palagio, wakipata mlo, lakini watu waliokuwemo ndani walijikuta wakiwatumbulia macho kutokana na vituko vya mastaa hao.

Ilielezwa, kivazi cha Bianca kiliwapa mshangao watu wengi hasa kutokana na kuonyesha sehemu kubwa ya umbo lake, lakini Kanye alionekana kufurahi huku aitumia simu yake kumrekodi video mpenzi wake.



## Sule Suebebe mwenda zake

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Dayo Adewunmi, maarufu kama “Sule Suebebe” amefariki dunia.

Muigizaji huyo wa Kiyoruba alifariki Jumatano wiki hii baada ya kuugua kwa miezi kadhaa.


Taarifa ya kifo chake imetolewa na muhubiri maarufu anayeishi katika mji wa Ibadan, Ademola Amusan, ambaye alisema Baba Suebebe alifariki hospitalini wakati akipatiwa matibabu.

## 2Baba kazidiwa mahaba

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Innocent Idibia, maarufu kama 2Baba, amesema mapenzi hufanya mtu kutenda jambo hata kama hakulipenda.

Akizungumza hivi karibuni, amesema yeye sio shabiki wa viopindi vya maisha halisi vinavyoonyeshwa kwenye televisheni, lakini amejikuta akiingia kutokana na mahaba aliyonayo

“Sitazami vipindi vya televisheni kuhusu maisha halisi, labda ikiwa mtu alikuwa anakitazama nilipoingia mahali fulani kutokana na mapenzi kama mimi,” amesema.





## Charly Boy hukujua hilo kosa?

MSANII wa muziki wa Agfrobeats kutoka Nigeria, Charly Boy, ameomba radhi baada ya kutoa maoni yasiyofaa kuhusu tukio la hivi karibuni la kuanguka kwa rais wa nchi hiyo Bola Tinubu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram mnamo, mkongwe huyo alikubali kuwa maoni yake yalikuwa potofu na hayakupaswa kwa kiongozi wa nchi.

“ Sote kwa wakati mmoja au nyingine tunafanya makosa na kujifunza, ninamuunga mkono rais ambaye hatakiwi kuumizwa baada ya tukio lile,” ameandika.

## Celine Dion aapa kutumbuiza

MWANAMUZIKI maarufu nchini Marekani, Celine Dion ametangaza kwamba hataruhusu ugonjwa wake kumzuai kupanda jukwaani na kuapa atatumbuiza hata kwa kutambaa.

Dion kwa sasa anapambana na ugonjwa wa Stiff Person Syndrome, ambao unashambulia misuli na kusababisha kusitisha shughuli yake ya muziki.

Katika mahojiano na mtangazaji wa runinga, Hoda Kotb, kwenye kipindi cha Today Show, msanii huyo mwenye umri wa miaka 56 alisema atatumbuiza tena mashabiki wake hata ikibidi kutambaa jukwaani na kutumia ishara za mikono kuwasiliana.







# Manyara yavuka lengo damu safi

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

BENKI ya Damu Salama imekusanya uniti 1,162 za damu katika mkoa wa Manyara, sawa na asilimia 109.64

Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa anayeshughulikia Huduma za Afya, Dk. Damasi Kayera, alisema kutokana na upungufu wa damu katika hospitali za umma, ili kukabiliana na hali hiyo, mahitaji ni chupa 15,150.

Dk. Kayera alisema mahitaji hayo ya damu salama kwa mkoa huo ni ya kipindi cha mwaka mzima.

Akizungumza jana mjini hapa wakati wa kilele cha Wiki ya Uchangiaji Damu Salama, Dk. Kayera alisema tangu kuanza kwa mwaka huu, tayari mkoa umekusanya damu kwa asilimia 76.

Dk. Kayera, alisema kazi ya kutoa elimu na kuchangia damu bado inaendelea ili jamii iongeze uelewa na kuchangia damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya watoto wachanga wenye uhitaji wa damu, wajawazito, majeruhi na makundi mengine ya jamii.

Kampeni hiyo ya kuchangia damu, ilianza Juni Mosi na ilihitimishwa jana.

Awali, Mkuu wa Idara ya Viwango na Ubora kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Dunstan Haule, alisema sifa za mtu kuchangia damu ni lazima awe na miaka 18 mpaka 65 na asiwe na magonjwa ya kudumu.

Haule alisema mwanamume anaweza kuchangia mara nne kwa mwaka, na mwanamke anaweza kuchangia damu mara tatu kwa mwaka.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, akizungumza na wakazi wa Mkoa huo alisema:

"Suala la uchangiaji wa damu ni sadaka na utoaji wa damu siyo dhambi tunasaidia watu wengine wenye uhitaji. .Niwaombe ndugu zangu, muwe na tabia ya kuchangia damu ili kusaidia kuokoa uhai wa watu wenye mahitaji ya damu."

# Mtafiti ahofia hatari sokwe mtu kutoweka

**Na Godfrey Mushi,**
ARUSHA

MTAFITI wa sokwe mtu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Simula Maijo, amesema wanyamapori hao wako katika hatari ya kutoweka hivi sasa kutokana na uharibifu mkubwa wa makazi yao.

Uharibifu huo ni ule unaosababishwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu hasa kilimo, ufugaji na uanzishwaji wa makazi holela ya binadamu katika maeneo yao ya asili.

Kwa mujibu wa Maijo, sokwe mtu ambao ni rafiki wa mazingira, kwa asilimia kati ya 60 na 80, chakula chao kikuu ni matunda.

"Sokwe ni mnyama adhimu Tanzania, ambaye kwa asili anapatikana katika mikoa ya Kigoma (Gombe na Mahale), Mkoa wa Katavi (Misitu ya Tongwe) na baadhi ya maeneo ya Rukwa (Kalambo).

"Tanzania ina Sokwe katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo, ambao siyo wa asili katika maeneo hayo.

"Kwa Tanzania Sokwe wanakadiriwa kuwa chini ya 2,500 kwa idadi. Na kati ya idadi hiyo, zaidi ya asilimia 75 wanapatika na kuishi katika maeneo ambayo yanapatikana nje ya Hifadhi za Taifa za Gombe na Mahale," alisema.

Aidha, mtafiti Maijo alisema sokwe ni mnyama wa kipekee na mwenye umuhimu mkubwa katika mifumo Ikolojia wanayopatikana, hivyo kuna uhitaji wa dhati kuhakikisha wanyama hao wanahifadhiwa ili kudumisha uwiano wa ikolojia wanayopatikana na kuishi.

Pamoja na mambo mengine, Maijo alisema sokwe ndiye mnyama pekee aliye na ufanano mkubwa wa vinasaba na binadamu. Taarifa za kisayansi, zinaonyesha kuwa sokwe anashahabiana kivinasaba na binadamu kwa zaidi ya asilimia 98.

Mtafiti huyo alifafanua kuwa katika uhifadhi, sokwe wanasaidia kusambaza mbegu mbalimbali kutokana na vyakula wanavyokula. Katika kula matunda ya mimea ambayo ni chakula chao, sokwe huwa wanameza pia mbegu za matunda hayo.

Utafiti unaonyesha mbegu iliyopita katika mfumo wa umeng'enyaji wa chakula cha Sokwe ina asilimia kubwa ya kuota ikilinganishwa na mbegu ambazo hazikupitia mfumo huo.

Akizungumzia upande wa uchumi, Mtafiti Maijo alisema sokwe wanachangia pato la taifa kupitia utalii wa picha.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Bia ya Serengeti, Obinna Anyalebechi wakivuta pazia kuzindua rasmi mradi mpya wa maji katika kijiji cha Kabila, wilayani Magu, mkoani Mwanza jana, unaofadhiliwa na kampuni hiyo na kutekelezwa na AFRIcai kwa kushirikiana na Wakala wa Maji safi na Usafi wa Mazingira (RUWASA), unaotarajiwa kunufaisha wakazi 12,000 wa kijiji hicho na cha N'gwamagoli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Spika EALA amlilia mbunge Mlozi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SIKU moja baada ya kutangazwa kifo cha Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Dk. Shogo Mlozi, Spika wa Bunge hilo, Joseph Ntakirutimana, amejitokeza na kusema wamepoteza mtu mahiri aliyekuwa ameweka nguvu zake katika kushughulikia masuala muhimu yanayowakabili kikanda.

Dk. Shogo, enzi za uhai wake alijenga hoja ndani ya EALA kwa wakati wote akipigia debe masuala ya ujumuishwaji maendeleo ya kiuchumi, biashara na ushirikiano wa kikanda.

Mbunge huyo, alifariki dunia Juni 13, mwaka huu, wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Kupitia taarifa yake iliyotumwa kwenye mitandao ya kijamii leo, Spika Ntakirutimana amesema mbunge huyo kutoka Tanzania alikuwa makini katika bunge hilo.

"Marehemu Mheshimiwa Dk. Mlozi alikuwa anatumikia awamu yake ya kwanza kama Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alikuwa kijana anayeheshimika na kuheshimiwa," alisema.

Alisema Dk. Shogo, alijijengea umaarufu zaidi kwa dhamira yake isiyoyumba katika kuwahudumia watu wa Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa Spika Ntakirutimana, shauku ya Dk. Shogo ilikuwa kubwa katika kukuza umoja na ushirikiano kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ilionekana katika kazi na utetezi wake ndani ya Bunge na kwingineko.

Aidha, alisema pia alijitolea kuendeleza malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki .

"Kupitia kifo hiki kwa kumpoteza Dk. Mlozi, ni hasara kubwa kwa Bunge la Afrika Mashariki na kwa ujumla wake, Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mawazo na sala zetu ziko pamoja na familia yake, marafiki, na wafanyakazi wenzake wakati huu mgumu,"alisema Spika huyo.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Sifa ya mke anayejua kutwanga, kupika inavyotoweka kwa kasi

## -Teknolojia imebadili kila kitu
## -Kutwanga kisamvu, kukuna nazi sasa wanatumia mashine

Na Adam Fungamwango

KILA miaka inavyozidi kwenda mbele, ndivyo teknolojia inavyozidi kurahisisha maisha. Hivi sasa kila kitu kinapatikana dukani kikiwa tayari kimeshakobolewa au kusagwa. Tena kwa bei rahisi tu. Unaweza kupimiwa, au ukakuta tayari kimefungwa kwenye mifuko. Unga, na nafaka zingine za kukobolewa zinanunuliwa zikiwa tayari, tofauti na zamani.

Na kwa sasa niseme tu hata tui la nazi linauzwa madukani, wakati zamani ni lazima nazi ikunwe kwenye kibao cha mbuzi.

Nakumbuka akinamama zamani walikuwa wanatwanga kisamvu kwenye kinu baada ya kukinunua sokoni, siku hizi wananunua kikiwa kimetwangwa tayari. Haya ni maendeleo, ingawa kuna watu wanasema imewafanya baadhi ya kinadada zetu kuwa wavivu sana, wasio na mazoezi kiasi cha kulazimika kwenda 'gym' kulipia kupunguza unene, kwani kutwanga chochote kwenye kinu, iwe kisamvu, mahindi, mpunga, kwa kinadada wa wakati ule yalikuwa ni mazoezi tosha yaliyowafanya kuendelea kulinda shepu zao kwa muda mrefu.

Kinamama enzi hizo, anasumbuka kuanika, mpunga au mahindi, baadaye ataita majirani wenzake watamsaidia kutwanga. Watakoboa mahindi, au mpunga na baadaye kuyapeleka mashineni.

Huko mashineni nako ni kazi ya kutwa nzima, maana wakati huo kulikuwa na foleni.

Miaka ya nyuma iwe mijini au vijijini, hadi mwishoni mwa miaka ya 1980, ilikuwa ngumu mno kupata moja kwa moja unga wowote ule ukiwa umesagwa.

Huko vijijini ndiyo kabisa, kwa sababu mahindi yakishavunwa yanawekwa kwenye vichanja vya kuhifadhia chakula. Halafu taratibu yanakwenda kusagwa ili upatikane unga, pale inapohitajika.

Sasa, miaka ya nyuma huko, tena hii ni tangu enzi za mababu zetu, moja kati ya sifa za mke bora, pamoja na mambo mengine ni umahiri wa kutwanga, kupika, kukuna nazi, kufua, na hata wakati mwingine kulima.

Mwanamke asiyejua kutwanga, iwe mahindi, mpunga, kukuna kazi kwa wale wakazi wa Pwani, kulima na kupika hafai au hana sifa za kuolewa.

Na wazazi walikuwa wanasisitiza hilo kwa vijana wao wanaotaka kuoa. Kijana anayempata msichana ilikuwa ni lazima ampeleke kwa wazazi wake akaishi japo wiki moja, wakati mwingine hata mwezi, lengo ni kuangalia utendaji wake wa kazi katika sekta iliyotajwa.

Akionekana mvivu, anavutavuta sana katika kazi, kupika kwake ni mtihani, hajui kukuna nazi kwa wale wa Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani, au kulima, anakosa sifa na wazazi wanamwambia kijana wao kuwa hatokuwa mke bora.

Hii iliwafanya vijana wengi kuwaacha wachumba zao bado wanawapenda, na kuwaumiza sana wasichana.

Ikumbukwe zamani neno la mzazi ilikuwa ni kama sheria, akisema amesema, haipingwi wala kuhojiwa, ni lazima mtoto atekeleze. Nadhani kwa sasa ingekuwa mtihani sana. Msichana unampenda, halafu unaambiwa eti umuache kwa sababu hajui kutwanga au kukuna nazi tu.

Kutokana na teknolojia kukua, hivi sasa hizo si sifa tena za mke bora kwa sababu kuna vitu vingi vimerahisishwa.

Sokoni kuna mashine za kusindika kisamvu, nazi, pia dukani sasa hivi wanauza tui la nazi, ili mradi tu maisha yamerahisishwa, siyo mpaka mwanamke afanye kazi kubwa ya kutwanga.

Akirejea kutoka sokoni, kila kitu kipo tayari anapika tu. Kwa maana hiyo vijana wa sasa wana vigezo vyao vingine kupata wake. Kila kitu na wakati wake. Vigezo vya kuwa mahiri sana kwenye mapishi, kutwanga, kulima, kujua kukuna nazi sasa havipo tena, vimepitwa na wakati, ingawa kama anavyo ni vizuri zaidi, ila si lazima.

Tuma meseji 0716 350534





HABARI KIMATAIFA

# ANC yakubaliana na DA kuunda serikali ya mseto

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

CHAMA tawala nchini Afrika Kusini cha African National Congress (ANC), kimesema kimepiga hatua katika juhudi za kuanzisha serikali ya umoja wa kitaifa baada ya kupata makubaliano na baadhi ya vyama.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Fikile Mbalula alisema chama chake bado hakiko tayari kutangaza makubaliano hayo.

ANC ilipoteza wingi wake wa wabunge kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30 katika uchaguzi wa Mei 29, baada ya kupata asilimia 40 ya kura zote.

Kutokana na matokeo hayo, ANC inahitaji kuungwa mkono na vyama vingine ili Rais Cyril Ramaphosa aweze kusalia madarakani.

Bunge jipya limeanza vikao vyake kuanzia jana kwa mara ya kwanza, linatarajiwa kumpigia kura Ramaphosa kuendelea na nafasi yake.

"Tunapozungumza hivi sasa tunajadiliana na vyama vya kisiasa," alisema Mbalula.

Alisema itakuwa kama kuhamia kituo cha kisiasa, kwa sababu vyama vilivyojitenga na ANC vilivyo upande wa kushoto vilisema havitajiunga.

Mbalila alieleza chama kilichoonyesha kuunga mkono wazo la serikali ya mseto ni Democratic Alliance (DA). Lakini bado vyama vyote viwili hawajaafikiana kuhusu maeneo ya kushirikiana.

"Kama DA ingepata baadhi ya vitu hivi inavyotaka ina maana ANC itakuwa imekufa," alisema.

DA ilishika nafasi ya pili katika uchaguzi huo kwa asilimia 22 ya kura.

Mpango wowote utakaojumuisha chama cha DA hautakubaliwa na miongoni mwa wanaharakati wengi wa ANC.

Chama hicho ambacho wanachama wengi ni wazungu ni mtetezi wa uchumi wa soko huria, ambapo kinakinzana na mila za mrengo wa kushoto wa ANC, na kina sifa ya kuwakilisha maslahi ya wazungu walio wachache.

ANC imeuita muungano huo kama Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU), lakini haikuweza kushawishi vyama vingine kikiwamo chama cha Rais wa zamani Jacob Zuma cha Umkhonto weSizwe (MK) na Economic Freedom Fighters (EFF) kinachoongozwa na Julius Malema.

Taarifa zilizopatikana jana jioni, zilieleza mjumbe kutoka chama cha DA, Hellen Zille, amethibitisha makubaliano yametiwa saini kuunda serikali ya muungano.

Vyombo vya habari kadhaa vya Afrika Kusini pia vinaripoti kuwa maafikiano yamefikiwa

**BBC**



Wakimbizi wa Sudan wakichota maji kutoka katika bomba lililokatika kwa ajili ya kunywa.Vita vinavyoendelea nchini humo vimeathiri miundombinu ya kijamii. **PICHA: REUTERS**

# Rais Tinubu asimulia alivyoanguka

**ABUJA,** NIGERIA

RAIS wa Nigeria Bola Tinubu, amezungumzia tukio la kuanguka kwake wakati akijiandaa kukagua gwaride, akisema jambo hilo ni la kawaida kwake kutokana na utamaduni wa kabila lake la Wayoruba. Kiongozi huyo aliteleza na kuanguka kwenye hafla ya miaka 25 ya demokrasia nchini humo. Tinubu mwenye umri wa miaka 72, alianguka alipokuwa akipanda ngazi ya gari la kumpeleka karibu na bustani ya Eagle Square jijini Abuja.

Jioni ya jana wakati akitoa hotuba kwenye chakula maalum, Rais Tinubu, alisema alibaini tukio la kuanguka kwake limesambaa katika mitandao ya kijamii.

"Mapema leo (jana) asubuhi, nilikuwa nimetawala kwenye mitandao ya kijamii. Wamechanganyikiwa kama nilikuwa nafanya buga au kufanya babanriga," alisema rais Tinubu. (Babanriga ni ngoma maarufu ya kitamaduni nchini Nigeria).

"Hata hivyo jana ilikuwa siku ya kusherehekea demokrasia huku nikifanya dobale [salamu ya Kiyoruba ya kusujudu kwa ajili ya wazee]. Mimi ni mvulana wa jadi wa Kiyoruba, nilifanya dobale yangu." Aliongeza na kusababisha vicheko kutoka kwa watu waliohudhuria.

**BBC.**

# Umoja wa Mataifa waitaka RSF kuacha kuizingira El-Fasher

**NEWYORK,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa limepitisha azimio linalotaka kukomeshwa kwa mzingiro wa kijeshi kwenye mji wa El-Fasher ulioko jimbo la Dafur nchini Sudan.

El-Fasher ndio mji mkuu pekee wa jimbo la Darfur linalotawaliwa na serikali ya Sudan ambako zaidi ya watu milioni moja wanaripotiwa kuzingirwa na vikosi vya RSF.

Azimio hilo limetaka kikosi cha wanamgambo wa RSF pamoja na jeshi la Sudan kusitisha mara moja mapigano na kuwezesha kumalizika kwa vita hivyo ambavyo vimedumu kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Baraza hilo limeelezea wasiwasi kuhusu machafuko yanayozidi kutanuka na ripoti za kuaminika zinasema kwamba wanamgambo wa RSF wanaendeleza machafuko ya kikabila katika mji mkuu huo.

Baada ya kura hiyo, balozi wa Uingereza katika Umoja wa Mataifa, Barbara Woodward, aliwaambia wajumbe kuwa kupitishwa kwa azimio hilo ni jibu la wazi kwamba wanamgambo wa RSF waondoe mzingiro.

"Kupitishwa kwa azimio hili kunatuma ujumbe wa wazi kwamba ni sharti wanamgambo wa RSF waache mara moja mzingiro wao katika El Fasher, na pia pande zote lazima zisitishe mapigano." Alisisitiza.

Mji huo ndio pekee salama unaowahifadhi watu waliokimbia machafuko na mashirika ya misaada yameonya kuhusu kuwepo kwa hali mbaya kutokana na mapambano yanayoendelea.

Nchi ya Sudan ilitumbukia kwenye machafuko mnamo Aprili 2023, wakati mvutano kati ya wakuu wa pande mbili za kijeshi uligeuka kuwa vita katika mji mkuu Khartoum na kisha kuenea hadi maeneo mengine ikiwemo Darfur.

Umoja wa Mataifa ulisema hadi sasa, zaidi ya watu 14, 000 wameuawa na wengine 33,000 wamejeruhiwa.

Miongo miwili iliyopita, Darfur ilihusishwa mara kwa mara na mauaji ya kimbari na uhalifu wa kivita, uliofanywa hasa na wanamgambo wa kiarabu Janjaweed.01:48

Takriban watu 300,000 waliuawa na wengine milioni 2.7 walilazimika kuyakimbia makazi yao.

Mnamo Januari mwaka huu, mkuu wa mashtaka katika mahakama ya kimataifa ya Jinai Karim Khan, alisema zipo sababu za msingi kuamini kwamba pande mbili husika katika machafuko ya sasa ya Sudan zimefanya uhalifu wa kivita dhidi ya ubinadamu au zimefanya mauaji ya kimbari katika jimbo la Darfur.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Meneja Huduma za Utangazaji wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi Andrew Kisaka, akitoa elimu kuhusu wajibu na majukumu ya vyombo vya habari katika kuelimisha umma wakati wa semina ya siku mbili ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura iliyoandaliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura (kulia) akikabidhi zawadi kwa Balozi wa Tanzania nchini Zambia, Lt. Jen. Mathew Mkingule, wakati alipomtembelea ofisini kwake, jijini Lusaka jana. IGP Wambura yupo nchini humo, ambapo juzi alikabidhiwa uenyekiti wa Shirikisho la Wakuu wa Majeshi ya Polisi kwa nchi za Kusini mwa Afrika (SARPCCO) kutoka kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi wa nchi hiyo, IGP Graphel Musamba ambaye amemaliza muda wake. **PICHA: JESHI LA POLISI**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mkizingo, Wilaya ya Mwanga walioanza kunufaika na Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe wakati akikagua mradi huo akiwa wilayani humo, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: OMR**



Mafundi wakichimba mfereji kwa ajili ya kutandika bomba la maji katika eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam jana ikiwa ni mikakati ya Serikali kusambaza huduma hiyo nchini kote. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Dereva wa bajaji, akiwa amepakia mizigo kupita uwezo wa chombo chake katika Barabara ya Morogoro, eneo la Ubungo Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-17

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Kitendo cha kuwa hajakamatwa mpaka sasa hakiwezi kuwapa usingizi waliofaya udhalimu huo, hivyo ili wakae kwa amani ni lazima wahakikishe, ama anatiwa mikononi wa polisi, au wanamuwahi kwa kummaliza. Kitu pekee ambacho anajivunia ni kwamba pande zote mbili hazijui pamoja na kwamba ametoroka, hawajui nini anataka kufanya. "Akili yao wao wanajua mimi nakimbia huku na kule kujifichaficha tu bila mpango, wamenoa." Akajisemea moyoni.

Asubuhi kulivyokucha aliondoka hapo moja kwa moja hadi kwenye zahanati moja maeneo ya Ilala.

Alimkuta mhudumu, akamwambia anajisikia vibaya, hivyo anaomba kitanda alazwe.

"Kwani unajisikiaje, huna nguvu?" "Siyo kama sina nguvu na kizunguzungu juu." Kamal alimjibu nesi aliyempokea. Hakukuwa na daktari kwa muda huo. Alipokuja alimpima lakini hakumkuta na ugonjwa wowote.

"Nadhani ni uchovu na kufanya kazi bila kumpumzika, lakini tumekupima kila kitu, unaonekana hauna tatizo." "Sawa lakini mimi dokta bado najisikia vibaya, tena kichwa ndiyo kabisa." "Basi endelea kumpumzika." Alipoondoka alipoondoka, alimwita nesi na kumwambia lengo lake ni kupumzika pale kwa siku tatu. Kabla nesi hajauliza sababu, alitoa noti tatu za shilingi efu kumi, akamkabidhi. Nesi akatabasamu. "Nataka nipumzike kwa sababu nina msongo wa mawazo, sitaki kurudi uraiani, nina matatizo kwenye familia yangu. Pia naomba unifunge bandeji kichwani kama mtu aliyeumia ili sura yangu usionekana vyema. Ndugu zangu wanaweza kunitafuta mahospitalini na zahanati wakanikuta hapa." Nesi akatii. Lengo halikuwa hilo. Ilikuwa ni kuishi pale kwa siku tatu bila bughuza. Polisi wanaweza kumsaka mhalifu sehemu zote, lakini siyo hospitalini na zahanati. Hata wanaomsaka hawawezi kuwa na wazo kuwa atakuwa anaishi hospitalini. Akili yake ilimtuma baada ya siku tatu atarejea kwenye hoteli aliyopanga Ubungo kuchukua mizigo yake ili ahamie sehemu nyingine.

*******************************

Tayari siku tatu alizokaa alikuwa ameshazoeana na nesi mmoja na daktari. Kwa sababu kila siku alikuwa akilipia kitanda shilingi elfu tano, hawakuhangaika tena kumhoji. Hata alipotimiza wiki nzima. Ilikuwa sasa ni kama sehemu ya kuongeza kipato.




**"Majuzi alikuja mtu mmoja mlikuwa mnaongelea hili suala, lakini inaonekana kabisa hakukuwa na usahihi katika uchunguzi wa madaktari."**

Alichofanya ni kurudi Ubungo ambako alikuwa ameweka mizigo yake fulani katika hoteli aliyofikia, akarejea kuishi hospitalini.

Akazoeana na nesi pamoja na daktari. Wao walimuona ni kama mtu mmoja ambaye ameikimbia tu familia yake, amemua kukaa sehemu ambayo haitaji bugudha. Kuhusu kushukiwa kuwa ni yule mtuhumiwa na mauaji ya mkewe, hakuwa na wasiwasi nalo kwa wale watu wawili.

Kwanza ile picha iliyotoka karibuni wiki nzima kwenye magazeti haikuwa na ufanano mkubwa na alivyo sasa.

Ilichukuliwa picha ambayo kwa wakati ule alikuwa amenyoa upara. Hilo ndilo kosa kubwa aliloliona kwa polisi waliokua wanamtafuta. Jinsi alivyo sasa, alikuwa na nywele nyingi, huku akipenda sana kuvaa miwani ya jua. Wakati mwingine akipiga na kofia juu.

Pamoja na hayo, bado alikuwa anatafakari jinsi gani anaweza kutoka pale, na atakapokwenda, kwani hakujidanganya kuwa atakaa hapo siku zote bila kugundulika.

Ndipo alipogundua kuwa daktari yule jina lake ni Dancun Shija, ambaye anafanya kazi katika hospitali ambayo ilifanya uchunguzi wa kifo cha mchumba wake, Mariamu. Akagundua kuwa ile ni zahanati yake binafsi.

Siku hizi baada ya madaktari huwa na zahanati au vituo vyao vya afya, licha ya kwamba ni waajiriwa na serikali katika hiospitali kubwa. Alisikia pia siku moja akiongea na mtu aliyekuja ofisini kwake, juu ya ripoti ya kifo cha mwanamke mmoja aliyesemekana ameuawa. Alijua kabisa anayezungumzwa ni Mariamu.

Alipatwa na faraja. Akajua tayari amepiga hatua ya pili kuelekea kuwapata wauwaji halisi. Alihitaji muda muafaka wa kumkabili daktari ili ampe angalau anachokijua yeye kuhusu sakata hilo.

*******************************

"Naitwa Kamal, mimi ndiye mchumba wa Mariamu, aliyeanguka kwa presha au kuuawa. Baadaye ikasemekana ameuawa na mpenzi wake." Alisema huku akikaa kwenye kiti kinachomkabili dokta Shija.

Kama alivyotarajiwa, dokta alipatwa na mshtuko mkubwa. Hakutegemea yule kijana ambaye ameshaanza kuwa rafiki yake, anayeonekana kuwa na nidhamu na ucheshi. Aliyekuja kudai anaumwa baadaye kuomba kulala ili kupunguza msongo wa mawazo wa nyumbani wake na familia yake, kumbe ndiye anayesemekana ni muuaji wa mchumba wake.

"Nadhani sasa dokta utaelewa au kufahamu kwa nini mimi nilikuja hapa kuomba 'hifadhi.' Ni kwa sababu ya kuhofia kukamatwa. Dunia nzima inajua kuwa mimi ni muuaji. Lakini ukweli uliopo moyoni mwangu ni kwamba mimi sijamuua mpenzi wangu. Nina simanzi ya kuuawa kwa mchumba wangu, walimwengu wakaniongezea uchungu mwingine wa kunisingizia uuaji."

"Kumbe wewe ndiye mchumba wa yule binti!?" Akauliza dokta kwa mshangao. "Hilo ni jibu dokta."

Akatikisa kichwa halafu akamalizia kwa kusema, "Pole sana kijana. Hata mimi najua kuwa mchumba wa yule msichana si muuaji." Jibu hilo lilimpa nguvu Kamal. Alijua kile alichokuwa anafikiria ni kweli.

"Majuzi alikuja mtu mmoja mlikuwa mnaongelea hili suala, lakini inaonekana kabisa hakukuwa na usahihi katika uchunguzi wa madaktari."

"Mimi mwenyewe nilikuja najiambia, kama nitabahatika kukutana na mchumba wa msichana yule ningemweleza ukweli wa hili suala. Mimi nafanya kazi kwenye ile hospitali. Niliwekwa kwenye uchunguzi wa pili, baada ya ule ya kwanza kutiliwa shaka."

"Enhee daktari, kwanza nataka uniambie, ule wa kwanza na wa pili upi ulikuwa sahihi?" "Wa pili!"

"Kwa nini?" Wa kwanza ulikuwa na shinikizo kutoka kwa watu fulani wenye uwezo. Walikuja wakamwaga pesa kwa baadhi ya madaktari wenzetu ili wapindishe uchunguzi. Na hao ndiyo walikuja kusema alianguka kwa kupatwa na presha ghafla barabarani akiwa anakimbia jogging alfajiri. Kelele zilivyopigwa na watu, pamoja na ndugu wa marehemu, kulikuwa na shinikizo kubwa, ikabidi madaktari wengine wateuliwe, siyo wale sasa. Ni sisi ambao tulikuja kugundua kuwa marehemu aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani. Wala hakuanguka kwa shinikizo la moyo." "Sasa umejuaje kama mimi siyo muuaji, wakati uchunguzi wa pili ulionyesha ameuawa?" Akaendelea kuuliza Kamal.

"Sisi wenyewe madaktari baada ya uchunguzi wa pili tukaanza kuulizana, ilikuwaje ikawa hivyo? Ndiyo tukapata taarifa za uhakika kuwa waliomuua ndiyo waliotumia pesa ili kupindisha uchunguzi wa kwanza. Na hao hao walitaka kushinikiza uchunguzi wa pili uwe kama wa kwanza, tukakataa. Tukautoa kama ilivyo. Tukapata taarifa sasa kuwa wale wale jamaa, wamekwenda kutoa pesa kwa baadhi ya askari polisi wasio waaminifu wamsingizie mtu kesi ya mauaji baada ya taarifa sahihi kutoka na kuwaridhisha ndugu na wananchi. Nilishangaa na kupatwa na simanzi niliposikia eti 'aliyepewa kesi ya kichwa', ni mchumba wake."

**Itaendelea Jumamosi**

# MBIO ZA UBINGWA LIGI KUU ZANZIBAR ZAKOLEA

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

VITA ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar imeendelea kushika kasi baada ya Zimamoto SC kuifunga Ngome FC mabao 4-3 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A, visiwani hapa juzi jioni.

Matokeo ya mchezo huo wa raundi ya 28 hayo yameifanya Zimamoto kufikisha pointi 61, akiwa nyuma kwa tofauti ya pointi moja na vinara wa ligi hiyo, JKU.

Mechi hiyo ilikuwa na ushindani kutokana na kila upande kutaka kufikia malengo, Zimamoto ikijiimarisha kwenye mbio za kuwania ubingwa wakati Ngome wao wanapambana kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo imebakisha raundi mbili kumalizika, endapo Ngome FC atashinda michezo yake iliyobakia atafikisha pointi 33, ambazo New City FC inazo na kwa sasa iko katika nafasi ya 11 kwenye msimamo huo.

Akizunguma na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohmed Hilali, alisema anaendelea kukiimarisha kikosi chake ili apate ushindi katika mechi hizo mbili zilizobakia.

Hilali alisema kikosi chake bado kipo katika mbio za kuwania ubingwa lakini malengo yao yatatimia endapo mpinzani wake atapoteza mchezo mmoja.

„Hivi sasa timu zote 16 zimebakisha michezo miwili, matumaini yangu ni kuendelea kupambana kusaka ushindi katika michezo hiyo, lakini vile vile kuwaombea anguko wapinzani (JKU) wetu," Hilal alisema.

Kocha huyo alisema tofauti wa alama moja katika mbio hizo ni kubwa hasa katika hatua waliyopo ambayo kila upande unapigania kushinda taji la Ligi Kuu Zanzibar.

„Michezo miwili iliyobakia ndio itakayoamua nani anakuwa bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu huu, na sisi bado tupo katika mbio hizo, hatujakata tamaa,"aliongeza kocha huyo.

Wakati huo huo Uhamiaji ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kundemba katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau B juzi jioni.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar atapata nafasi ya kukiwakilisha kisiwa hicho katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku bingwa wa Kombe la ZFF akienda kupambana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Mshambuliaji wa Mapinduzi Queens ya Njombe (kulia), akimtoka nyota wa JMK Park katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza Wanawake (WFDL), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Fountain Gate jijini, Dodoma jana. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: TFF**

# Biashara: 'Tutapaki basi' Tabora

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Amani Josia, amesema watacheza kwa kujilinda zaidi katika mechi ya marudiano dhidi ya Tabora United ili kuhakikisha wapinzani wao Tabora United hawapati bao.

Biashara United ilipata ushindi wa bao 1-0 nyumbani, itawafuata Tabora United katika mechi ya marudiano itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Josia aliliambia gazeti hili ameandaa mikakati ya kwenda kuimalizia mechi kwa kutengeneza mfumo mzuri wa ulinzi, kushambulia kwa kushtukiza, na ikiwezekana wao ndiyo waanze kupata bao.

Kocha huyo alisema atawaandaa wachezaji wake kisaikolojia kwa sababu watakuwa wapo ugenini mbele ya mashabiki wa timu pinzani.

"Tunahitaji kwenda kujilinda zaidi katika mechi ya marudiano, pia kupata bao angalau moja la ugenini, ikiwezekana sisi ndiyo tutangulie, jukumu lingine ni kuwatengeneza wachezaji kisaikolojia, ndiyo itakayotubeba, kwa sababu hii mechi haijaisha," Josia aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa Tabora United, Barnard Fabiano, aliyechukua nafasi ya Masoud Djuma, aliyetimuliwa alionekana ana imani ya kupata matokeo chanya katika mechi ya nyumbani.

"Mechi imeisha, wenzetu wamepata bao moja, tunawapongeza, nina imani na sisi tutapata bao moja au zaidi nyumbani," alisema Fabiano.

## Wanawake Songwe, Mbeya kuchaguana leo

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Songwe kinatarajia kufanya uchaguzi mkuu leo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Songwe (SOREFA), Emmanuel Mwambinga, alisema maandalizi yote kuelekea uchaguzi huo yamekamilika.

Mwambinga alisema anaamini uongozi mpya utakaoingia madarakani utasaidia kuhamasisha mpira wa wanawake kuchezwa katika wilaya zote za mkoa huo.

"Taratibu na kanuni zote za uchaguzi kama ilivyoelekezwa zitafuatwa, tunaamini wajumbe watatumia haki yao kuchagua viongozi," alisema Mwambiga.

Wakati huo huo, Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Mbeya (MRWFA), kitafanya uchaguzi wake leo.

"Tunaendelea vizuri, wagombea pia wamejitokeza katika nafasi zote zilizotajwa kwa mujibu wa katiba, tunaamini uongozi utakaoingia madarakani utaleta mapinduzi kwenye mkoa wetu," alisema Kubaja.

## Mabondia Dar 'dabi' waendeleza majigambo

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Said Bwanga amesema yuko fiti na anaamini atampiga mapema mpinzani wake Said Mkola katika pambano litakalofanyika Juni 29, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika usiku huo uliopewa jina la Dar Boxing Derby.

Bwanga aliliambia gazeti hili anaendelea vyema na mazoezi na ameshajua udhaifu wa mpinzani wake.

"Nimejiandaa kwa muda mrefu kwa ajili ya kuhakikisha nitashinda pambano hili, naomba mashabiki wangu wajipange kushuhudia ninavyomtwanga Mkola, sitampa nafasi ya kunizoea," Bwanga alisema.

Naye Mkola alisema hana muda wa kuzungumza na badala yake atakwenda kuonyesha vitendo ulingoni kwa sababu amejiandaa kuweka rekodi katika pambano hilo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE, BAYERN VITANI
NEWCASTLE United na Bayern Munich zilikuwa klabu za kwanza kuwasiliana na Crystal Palace zikitaka kumsajili winga raia wa Ufaransa, Michael Olise. mwenye umri wa miaka 22. (***Athletic***)

### CHELSEA YAMTAKA OLISE
CHELSEA nao wameingia katika vita ya kuwania huduma ya nyota wa Crystal Palace, Michael Olise. (***Mirror***)

### MADUEKE ANUKIA CHELSEA
MCHEZAJI wa kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 22 na Chelsea, Noni Madueke, yuko kwenye orodha ya wanaowaniwa na Newcastle United huku klabu hiyo ikiwa na mpango wa kumnunua winga mpya wakati dirisha la uhamisho wa wachezaji litakapofunguliwa. (***i Sport***)

### VAN DIJK TAJIRI MPYA
KLABU ya Al Nassr inayoshiriki Ligi Kuu Saudia, inataka kumfanya beki wa Liverpool na timu ya taifa ya Uholanzi, Virgil van Dijk kuwa beki anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani. (***Marca***)

### DE LIGT KUTUA UNITED
KLABU ya Manchester United inamfuatilia kwa karibu beki wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt, mwenye UMRI wa miaka 24. (***Sky Sports Germany***)

### TODIBO SOKONI ENGLAND
KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumsajili, Jean-Clair Todibo, mwenye umri wa miaka 24. (***Mail***)

### ZIRKZEE AGOMBEWA ULAYA
MSHAMBULIAJI wa Bologna Mholanzi Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 23 yuko kwenye rada za Manchester United msimu huu wa joto, lakini wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa AC Milan na Juventus. (***Telegraph***)

### YORO AGEUKA LULU
LIVERPOOL na Manchester United zote zinamsaka beki wa kati wa Lille Mfaransa Leny Yoro, mwenye umri wa miaka 18, lakini Real Madrid pia wanamtaka. (***Athletic***)

### SPURS YAMWANIA ABRAHAM
KLABU za Tottenham, Aston Villa na West Ham zinavutiwa na mshambuliaji wa Roma na Timu ya Taifa ya England, Tammy Abraham, mwenye umri wa miaka 26. (***Telegraph***)

### DURAN KUONDOKA VILLA
KLABU ya Aston Villa inahitaji pauni milioni 40 ili kumnunua mshambuliaji, Jhon Duran, huku Chelsea ikiwa kwenye mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. Raia huyo wa Colombia amecheza mechi tatu pekee za Ligi Kuu England tangu ajiunge nao Januari 2023. (***Times***)

### MOURINHO AMTAKA HOJBJERG
KOCHA mpya wa Fenerbahce, Jose Mourinho, anataka kumsajili kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye miaka 28 kutoka Tottenham. (***Takvim***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KANE : WAJERUMANI WAIPA TAJI ENGLAND

**BERLIN,** Ujerumani

## Ni la michuano ya Euro 2024 kwa sababu wanaamini nahodha huyo...

HARRY Kane anaamini baadhi ya mashabiki wa Ujerumani wanatumaini ya ,siri' kuwa England itaimarika kwenye Euro 2024 kwa sababu ya msimu wake wa kwanza akiwa na Bayern Munich.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 hajashinda kombe lolote akiwa na Bayern Munich huku Bayer Leverkusen wakishinda taji lao la kwanza la Bundesliga lakini nahodha huyo wa England alifunga mabao 44 katika michezo 45 kwenye michuano yote kufuatia uhamisho wake wa Euro milioni 120 kutoka Tottenham.

England na wenyeji Ujerumani ni miongoni mwa timu zinazopewa nafasi kubwa ya kushinda fainali za msimu huu wa kiangazi na Kane alisema: "Mapokezi niliyopata tangu nikiwa Bayern yamekuwa ya ajabu na tangu nikiwa katika hoteli ya timu nimekuwa na baadhi ya wafanyakazi wanakuja kunisalimia.

> **"Sisemi wanataka England ishinde, lakini nadhani wana nafasi nzuri kwetu -- sasa niko hapa -- na hiyo ni nzuri."**

Kane pia alifichua mchezaji mwenzake wa Bayern, Thomas Müller, alimwachia ujumbe katika Kituo cha England cha Weirmarer Land Golf and Spa Resort mjini Blankenhain.

Ujerumani walitumia uwanja huo kwa michezo yao miwili ya kujiandaa kabla ya kuhamia mji wa Kaskazini mwa Bavaria wa Herzogenaurach kwa ajili ya mashindano hayo na Kane alisema: "Tommy aliniachia dokezo kidogo, kwa sababu walikuwa hapa wiki chache zilizopita.

"Alisema uwanja wa gofu ni mzuri lakini hali ya hewa imekuwa si nzuri sana! Inaonekana ya kustaajabisha, hoteli ni ya ajabu na kuwa Ujerumani ni nyumbani kidogo kutoka nyumbani."

Kane anatazamiwa kuwa nahodha wa England katika mechi yao ya ufunguzi ya Kundi C dhidi ya Serbia itakayochezwa kesho mjini, Gelsenkirchen.



# UNITED KUWEKA KIKOMO MADARAKA YA TEN HAG

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wanatarajia, Erik ten Hag, hatahusika moja kwa moja katika usajili wakati mazungumzo ya mkataba mpya yatakapoanza, huku uamuzi umefikia Mholanzi huyo atasalia Old Trafford.

Tathmini ya baada ya msimu mpya ilifanywa na uongozi mpya wa michezo wa United baada ya kumaliza nafasi ya nane katika Ligi Kuu England na ushindi wa Kombe la FA, ambayo ilikuwa kuamua ikiwa Ten Hag ndiye angekuwa mtu wa kuinoa timu katika enzi mpya au klabu ingeenda upande mwingine.

Ingawa United inaaminika kuwa katika mazungumzo na mbadala kadhaa - ikiwa ni pamoja na Thomas Tuche, Kieran McKenna na Thomas Frank, Mkurugenzi wa Michezo wa INEOS, Sir Dave Brailsford, Msaidizi Mkuu wa Sir Jim Ratcliffe, ametajwa na ripoti moja kama mtu anayetamani sana kubaki na Hag.

Kwa mujibu wa EPSN mada mbili muhimu katika mazungumzo yaliyopangwa yatazingatia kupunguza ushawishi wa Ten Hag juu ya kusajili na kurekebisha muundo wa wafanyikazi wake wa kufundisha.

Tangu kuwasili kwake, kocha huyo ameshikilia mamlaka ya kura ya turufu juu ya uhamisho unaoingia na kutoka.

Huku Andre Onana, Lisandro Martinez na Antony, United wametumia fedha nyingi kununua wachezaji ambao amefanya nao kazi hapo awali, huku wakiwalenga wengine kama Frenkie de Jong na Brian Brobbey.

Klabu hiyo pia sasa inajiondoa katika nia ya kumnunua, Matthijs de Ligt, nyota mwingine wa zamani wa Ajax ya Ten Hag.

Katika muundo mpya unaopendekezwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 54 bado atakuwa na „sauti" ya uhamisho, lakini jukumu lake hasa ni kufundisha na kusimamia kikosi cha wachezaji ambacho kinaonekana dhahiri kuwa kimekusanywa kwa ajili yake na idara ya uajiri maalum inayoongozwa na Mkurugenzi, Dan Ashworth.

Kufikia sasa, usajili wa majira ya joto umeongozwa na mkurugenzi mpya wa ufundi, Jason Wilcox na Skauti Mkuu, Steve Brown, huku Ashworth bado hajajiunga na kilabu kutoka Newcastle United.

# Madrid yakomaa kumsajili Davies

**MADRID,** Hispania

BAADA ya kupata saini ya Kylian Mbappé, lengo linalofuata la Real Madrid ni kujaribu kumsajili beki wa pembeni wa Bayern Munich, Alphonso Davies, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada unaisha mwaka 2025, na ESPN iliripoti Januari, Madrid ingemsajili ikiwa mchezaji huyo angeamua kutoongeza mkataba na Bayern Munich.

ESPN imeripoti uhusiano kati ya Madrid na Davies ni „bora" na klabu inasubiri mchezaji huyo na Bayern Munich, kuamua juu ya hatua zao zinazofuata kabla ya kumsajili.

Davies anakagua ofa ya hivi punde ya Bayern ya kuongeza mkataba, vyanzo viliiambia ESPN, lakini masharti hayo ni mbali na yale ambayo mchezaji huyo angezingatia kukubali kuendelea na wababe hao wa Bundesliga.

Davies alikuwa na msimu mgumu akiwa na Bayern Munich, ambao wamemteua Vincent Kompany baada ya kutafuta kocha mpya kwa muda mrefu.

Bayern Munich walimaliza kampeni bila taji, na wakatolewa na Madrid katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa, huku Davies akitokea benchi na kufunga katika mechi ya mkondo wa pili Santiago Bernabéu.

Madrid haitalipa ada ya uhamisho ya juu kwa mchezaji ambaye angepatikana kwa uhamisho wa bure katika muda wa miezi 12. Mnamo Januari, ESPN iliripoti Madrid haitakuwa tayari kwenda zaidi ya euro milioni 35.

Hata hivyo mabingwa hao wa LaLiga na Ulaya pia wanataka kuepuka kuharibu uhusiano wao na Bayern Munich, chanzo kilisema.

Madrid wana matumaini kuhusu nafasi yao ya kumsajili Davies, lakini watafanya hivyo iwapo tu Bayern Munich watakubali kufanya mazungumzo kuhusu bei ambayo inaendana na bajeti yao msimu huu wa joto.

Davies mwenye umri wa 23, anaonekana kama nyongeza muhimu kwenye kikosi.



# Edin Terzic abwaga manyanga Dortmund

**DORTMUND,** Ujerumani

KOCHA aliyeipeleka fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Borussia Dortmund, Edin Terzic, ameachia wadhifa wake ndani ya kikosi hicho.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 41 aliisaidia Borussia Dortmund kutinga fainali hiyo kwa mara ya kwanza ndani ya miaka 11.

Walipoteza dhidi ya Real Madrid kwenye Uwanja wa Wembley, huku Dortmund pia wakimaliza nafasi ya tano katika Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga.

Terzic aliiongoza Dortmund kwa vipindi viwili tofauti, kimoja akiwa kocha wa muda kibarua kilichoanza mwishoni mwa msimu wa 2020/21, kabla ya kurejea kama kocha wa kudumu msimu wa 2022/23.



HABARI MICHEZO

## Rais Samia awapa Taifa Stars 110m/-

INATOKA UK. 24

wake wanacheza soka la kulipwa nje ya Afrika.

Alisema timu hiyo itaendelea na maandalizi yake katika michezo mingine miwili ya mashindano hayo itakayochezwa ifikapo Machi, mwakani.

"Mwakani mwezi wa tatu tutakuwa na michezo miwili ambapo mchezo wa kwanza tutacheza dhidi ya Congo Brazaville utakaochezwa Dar es Salaam ukifuatiwa na ule wa Morocco, ninaomba Watanzania waendelee kuiunga mkono timu yetu, „ alisema waziri huyo.

Nahodha wa timu hiyo, Himid Mao, alimshukuru Rais Samia kwa kuwapa bonasi hiyo.

"Ilikuwa ni safari ya mafanikio, tulipata zaidi ya tulikokitarajia, ilikuwa mechi ngumu na ugenini, tunawashukuru Watanzania wote kwa maombi, waliokuwa uwanjani na waliotuangalia kwenye televisheni," Mao alisema.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Morocco, alisema wachezaji wake walifuata vyema maelekezo aliyowapa na hiyo ndio sababu ya kupata ushindi.

"Ninawapongeza wachezaji kwa kazi kubwa waliyoifanya na kupata ushindi ambao umetufanya tushike nafasi ya pili tukiwa na pointi sita," alisema Morocco.

Bao pekee la Stars katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko Ndola lilifungwa na straika wa KMC FC, Waziri Jr, dakika ya tano.

# SAIDO, DJUMA KUIBEBA COASTAL MICHUANO CAF

**Na Adam Fungamwango**

COASTAL Union imeanzisha mazungumzo na wachezaji, Saido Ntibazonkiza wa Simba na aliyekuwa beki wa Yanga, Djuma Shaaban, kwa ajili ya kuwasajili kuelekea msimu mpya wa mashindano, imefahamika.

Coastal Union ilimaliza katika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ulioisha na imeanza kuimarisha kikosi kwa ajili ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, amekiri wameanza mazungumzo na beki huyo Mkongomani, Djuma, lakini kusema lolote kuhusiana na Saido.

Sabri alisema wachezaji hao ni wazoefu katika mashindano ya kimataifa na uamuzi wa kuwasajili umezingatia kupata msaada wao kuendelea msimu mpya wa mashindano.

"Ni kweli tupo katika mazungumzo na Djuma, ni mchezaji mzuri, mzoefu katika mechi za kimataifa. Unajua tangu tulipopata nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho, tayari kama klabu tukatambua mahitaji yetu yataongezeka, kuanzia gharama, wachezaji na hata muda utakuwa finyu, hivyo tuko kwenye mikakati kuhakikisha tunashiriki vyema na hatusindikizi kwa kusajili wachezaji bora," alisema Sabri.

Aliongeza wachezaji wao watarejea kuanza mazoezi Juni 20, mwaka huu badala ya Juni 28, kama walivyoelezwa wakati wanaenda mapumzikoni.

"Hatuwezi kumwacha Kocha, David Ouma ambaye amewafanya kucheza mechi za kimataifa mara ya kwanza tangu 1988. Ni kocha aliyetutoa mbali, tulikuwa ni timu ya kucheza ili tusishuke daraja, lakini ametupeleka Kombe la Shirkisho, tutaendelea kuwa naye na anakidhi vigezo," Sabri aliongeza.




Wachezaji wa Azam FC wakishangilia bao katika mechi ya Ligi Kuu Bara msimu wa 2023/2024 uliomalizika hivi karibuni dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Isamuhyo, Dar es Salaam. Azam ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## *Aziz Ki, Diarra kuifilisi Yanga*

INATOKA UK. 24

Aliongeza Yanga inafanya mchakato wa usjaili kwa umakini mkubwa na haufanyiki kwa kufuata na mihemko.

"Tutamsajili mchezaji yoyote tunayemhitaji, niwaambie mashabiki na wanachama wa Yanga, uongozi wao uko makini katika usajili, na hatuingizwi mkenge na baadhi ya wachambuzi, tutakachofanya ni kusajili wachezaji ambao watakiongezea thamani na ubora kikosi tulichokuwa nacho," alisema ofisa huyo.

Hata hivyo, Kamwe alisema Yanga bado haijaamua kama itashiriki mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Julai 6 hadi 22, mwaka huu hapa nchini.

Tayari Azam imeshatangaza kujitoa kushiriki michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), huku wawakilishi wengine kutoka Bara wakiwa ni Simba na Coastal Union.

"Bado hatujafikia uamuzi, kila kitu kitawekwa hadharani tutakapofikia uamuzi," alisema kwa kifupi Kamwe.

Habari zilizopatikana jijini zinasema mbali na kumtaka kwa udi na uvumba, straika, Prince Dube, ambaye bado ana magogoro wa kimkataba na waajiri wake, Azam FC, Yanga ipo mbioni kumalizana na Charve Onoya, kiungo mkabaji na kiungo mshambuliaji, Agee Basiala, wanaokipiga katika klabu ya AS Maniema ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).



Mabingwa hao wa Kombe la FA wanatajwa pia wanakaribia kumalizana na beki wa kati, Chadrack Boka kutoka Saint Eloi Lupopo ya DRC.

# TFF yazikumbusha timu kulipa madeni

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limezikumbusha klabu zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao kukamilisha taratibu zote zinazotakiwa na Shirikisho la mchezo huo Afrika (CAF).

Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na Azam FC zitashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Simba na Coastal Union zitapeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema jana mwisho wa kukamilisha mchakato huo ni leo na shirikisho hilo linazitaka klabu zitakazoshiriki mashindano ya CAF kuhakikisha zinajiandaa vyema.

"Klabu itakayotimiza masharti ya leseni za klabu ndio itakayoruhusiwa kushiriki mashindano hayo. TFF inazikumbusha klabu zote kufanya maombi kwa wakati, hakutakuwa na muda wa ziada baada ya tarehe ya mwisho," alisema Ndimbo.

Ofisa huyo aliongeza klabu zinazodaiwa na makocha, wachezaji au mfanyakazi mwingine itatakiwa kumaliza deni haraka ili watimize sifa ya kushiriki mashindano hayo ambayo mechi za awali zitachezwa kati ya Agosti 13 na 15, mwaka huu.

Yanga na Simba zitaanzia ugenini katika raundi ya pili ufikapo Septemba wakati Azam na Coastal Union wao wataanza kwenye hatua ya awali na michezo yao ya kwanza itachezwa nyumbani.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Juni 15, 2024



UK. 21

Kane : Wajerumani waipa taji England



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya England wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Kundi C ya mashindano ya Euro 2024 dhidi ya Serbia itakayochezwa leo usiku.**PICHA: MTANDAO**

# Rais Samia awapa Taifa Stars 110m/-

**Na Shufaa Lyimo**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. milioni 110 kwa Timu ya Taifa (Taifa Stars), baada ya kuwafunga Zambia (Chipolopolo), bao 1-0 katika mechi ya Kundi E ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia zitakazochezwa mwaka 2026.

Ushindi huo uliifanya Stars ifikishe pointi sita sawa na vinara wa kundi hilo, Morocco, ikiwa imecheza mechi tatu.

Akizungumza baada ya timu hiyo kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema Rais Samia aliahidi kutoa fedha Sh. milioni 100 kama motisha kwa wachezaji endapo watapata ushindi wowote.



Ndumbaro alisema pia na kiasi kingine cha Sh. milioni 10, kinatokana na ahadi ya ‚Goli la Mama'.

„Hii ni ahadi ambayo aliitoa Rais Samia wakati timu yetu inajiandaa kuelekea nchini Zambia ikiwa ni kutoa motisha kwa wachezaji kutokana na kazi kubwa waliyoifanya, „ alisema Ndumbaro.

Waziri huyo pia aliwapongeza wachezaji kwa kufuata vyema maelekezo waliyopewa na benchi lao la ufundi na kuongeza haikuwa kazi nyepesi kuifunga Zambia kutokana na asilimia kubwa ya wachezaji

INAENDELEA UK. 23

# Aziz Ki, Diarra kuifilisi Yanga

## ●●● Uongozi waahidi kutumia nguvu zote kuwabakisha huku ikishusha...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha la usajili wa wachezaji limefunguliwa rasmi leo, uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga unasisitiza nyota wake, Stephano Aziz Ki na kipa chaguo la kwanza, Djigui Diarra, wataendelea kubakia katika kikosi chao, imeelezwa.

Nyota mwingine ambaye Yanga inakaribia kumbakiza ili kupata huduma yake ni Pacome Zouzoua.

Nyota hao watatu wamemaliza mkataba wa kuwatumikia Yanga, na mabosi wanaendelea kukamilisha mazungumzo ili watie saini mikataba mipya, huku kukiwa na tetesi wanawindwa na vigogo mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema klabu hiyo itatumia kila rasilimali yake ili kuhakikisha inawabakisha wachezaji nyota wote walioipa mafanikio timu yao kwenye msimu uliopita.



Kamwe alisema pia mabosi wa klabu hiyo wako katika hatua za mwisho za kusajili nyota wapya ili kukiongezea nguvu kikosi chao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ofisa huyo amewataka wanachama na mashabiki wa Yanga kutokuwa na wasiwasi wa kuondokewa na nyota wao na waelewe kipindi hiki huongozwa na propaganda.

"Wanachama na mashabiki wa Yanga wamekuwa na furaha na amani kwa kipindi chote cha msimu, hivyo wasikae kwa kusononeka kipindi hiki kutokana na yanayosemwa watapoteza baadhi ya wachezaji wao nyota," alisema Kamwe.

Aliongeza tayari wameshaanza kuifanyia kazi ripoti ya benchi la ufundi lililoko chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi na watampa kila kitu ambacho ameelekeza kwa sababu wanataka kufikia malengo.

"Kwa sasa tunaifanyia kazi ripoti ya benchi la ufundi juu ya kukiboresha kikosi chetu, kwanza kabisa kila mchezaji wanamhitaji abaki kikosini, atabaki, uongozi utafanya hivyo, kwa hiyo wanachama na mashabiki wetu hawatakiwi kuwa na wasiwasi wowote, atakayeondoka ujue hahitajiki.

Kila aliyeifanyia timu kuwa tishio msimu uliopita tutatumia nguvu zetu zote tulizonazo kumbakisha, tunataka kutengeneza timu tishio zaidi msimu ujao kuliko hii iliyopita," Kamwe alisema.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >